




**Hofu** yatawala ng'ombe kuchinjwa kwa misumeno

UKURASA 4





# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Mei 22, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580953

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


## ALABA KUCHEZA FAINALI YA UEFA

UKURASA 21

# Rais Samia aonya nidhamu ya woga

UKURASA 2



Rais, Samia Suluhu Hassan akimwapisha Balozi Adadi Rajabu, kuwa Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Umma katika hafla fupi iliyofanyika Ikulu Chamwino, Jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Sweden yamwaga mabilioni fedha kusaidia ubunifu

UKURASA 3



## Kitimtimu NCCR kumsimamisha uenyekiti Mbatia

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA KAZI HAIJAKWISHA BARA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6



Baadhi ya watumishi wa Taasisi ya Usimamizi wa Fedha (IFM), wakiokoa baadhi ya mabaki ya vitu mbalimbali vilivyonusurika kuteketea kwa moto baada ya ofisi ya taasisi hiyo kuungua moto, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rais Samia aonya nidhamu ya woga

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameonya tabia ya baadhi ya watumishi wa umma kuwa na nidhamu ya uwoga badala yake wafanye kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

Amesema nidhamu kwa baadhi ya watumishi wa umma inakuwapo pale tu wanapotiwa vitisho lakini vitisho vikiondoka, nidhamu hiyo nayo inatoweka.

Rais Samia alibainisha hayo jana Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma baada ya kuwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua, wakiwamo wa Tume ya Utumishi wa Umma.

"Watumishi wetu hawajielewi. Nidhamu yao mpaka wapate vitisho, wakipata vitisho nidhamu inakuwepo, vitisho vikiondoka nidhamu hakuna.

"Sasa tunataka watumishi ambao watakuwa wana itikadi moyoni mwao kuwa mimi ni mtumishi wa umma 'ethics' (maadili) zangu (yangu) ni hizi. Nidhamu yangu mstari ni huu hapa," alisisitiza Rais Samia.

Kutokana na hali hiyo, aliitaka Tume ya Utumishi wa Umma wakalisimamie sana suala la nidhamu kwa watumishi pamoja na mambo ya kimuundo.

Pia alisema hali ya kushuka kwa nidhamu kwa watumishi inatokana na kutokuwapo na mafunzo ya mara kwa mara ya kada mbalimbali za utumishi wa umma.

"Nakumbuka mimi na Haule tulivyokuwa IDM (Mzumbe) kila baada ya muda tulikuwa tunaona makatibu wakuu, wakurugenzi kina nani walikuwa wanaingia pale na wana mabweni yao maalum. Sisi hatusogei huko, tunasema wakubwa wameingia. Walikuwa wanakuja na kuondoka, wanapata kozi fupifupi za mafunzo za kuwakumbusha wajibu wao wakiwa kazini.

"Jambo ambalo kwa muda mrefu limekufa lilikuwa linaendelezwa kidogo kidogo lakini baadaye likaachwa kabisa. Kwa maana hiyo, watumishi wa umma wamejikalia tu, wanakwenda tu, wanapandishwa vyeo bila kupata mafunzo yoyote yale. Kwa hiyo watu wanakwenda tu, naomba mkalisimamie sana suala hili," alisema.

Pia alisema Tume ya Utumishi inao wajibu wa kuhakikisha inarudisha nidhamu katika utumishi wa umma na uwajibikaji.

"Kwa sababu mtu unamwongezea tu mavyeo bila kumpa mafunzo, juzi wamefurahi wamepanda vyeo kwa mseleleko lakini huo mseleleko maana yake hawajui. Mtu kapanda ngazi mbili hadi tatu kwa pamoja lakini wajibu wake nini? Anapokwenda hajui, naomba myasimamie sana sana," alisisitiza.

Vilevile, aliitaka Tume ya Utumishi kwenda kusimama katikati bila upendeleo kwa kuwa Watanzania wote ni sawa na wenye sifa pekee ndiyo watatakiwa kwenda.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza katika hafla hiyo, alimpongeza Rais Samia kwa kupandisha mishahara ya watumishi.

Alisema Bunge ambalo kazi yake ni kuisimamia na kuishauri serikali, linampongeza Rais kwa kusikia kilio cha watumishi ambacho kimekuwepo kwa muda mrefu.

"Mheshimiwa Rais, sisi kama Bunge tunatoa pongezi zetu kwako kwa hatua hii uliyoichukua ambayo hata sisi tumekuwa tukiizungumzia kama wawakilishi wa wananchi ni jambo kubwa sana sana na tunakupongeza sana," alisema Dk. Tulia.

Pia alimpongeza kwa kuitangaza nchi kupitia filamu ya Royal Tour ambayo inawezesha kukua kwa sekta ya utalii nchini na kuliongezea taifa mapato.

"Lakini Mheshimiwa Rais ulipokuwa kwenye ziara yako ya kikazi Tabora hivi karibuni ulipata mapokezi makubwa sana hali hii inamaanisha kuwa watanzania wengi wanaguswa na namna unavyo fanya kazi yako hasa katika miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara"alisema

Hata hivyo, alisema Bunge linaendelea na jitihada za kutoa elimu kwa wabunge ili kuondoa migogoro iliyopo baina ya wabunge na wakurugenzi.

"Mheshimiwa hili ulishatoa maagizo lakini sisi kama bunge lazima pia tutoe elimu kwa wabunge wetu ili kila mmoja afanye kazi yake bila kumwingilia mwingine. Lakini pia tunaendelea kuisimamia na kuishauri serikali kama ilivyo wajibu wetu," alisema.

# Kitimtimu NCCR Mbatia kusimamishwa uenyekiti

**Na Beatrice Shayo**

KITIMTIMU kimeibuka ndani ya NCCR Mageuzi baada ya Halmashauri Kuu ya chama hicho kutangaza kumsimamisha Mwenyekiti wake, James Mbatia, kutojihusisha na shughuli zozote pamoja na Makamu Mwenyekiti Bara, Angelina Mtahiwa, hadi mkutano mkuu utakapoitishwa ili wajieleze kuhusiana na tuhuma zinazowakabili.

Wakati hayo yakitokea, uongozi wa chama hicho kupitia kwa msemaji wake, umesema kilichofanywa ni uhuni na kwamba Mbatia bado ni mwenyekiti halali wa chama hicho.

Uamuzi huo ulifanyika jana kutokana na tuhuma mbalimbali zinazodaiwa kuwakabili viongozi hao, ikiwamo kugombanisha viongozi na kulazimisha kujiuzulu.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya NCCR-Mageuzi na Mwenyekiti wa azimio hilo, Joseph Selasini, ndiye aliyetangaza maazimio hayo ya kusimamishwa kwa viongozi hao, na kueleza kuwa pia wamelivunja Baraza la Wadhamini la NCCR na kuteua wajumbe wapya ambao watasajiliwa kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa.

Akisoma maazimio ya halmashauri kuu, Selasini alitangaza kumsimamisha Mbatia katika wadhifa huo kwa kile alichoeleza ni kutokuwa na uhusiano mzuri na makatibu wake.

Selasini alisema sababu nyingine ni Mbatia anatuhumiwa kwa kukisababishia chama hicho kisishiriki mikutano mbalimbali iliyoitishwa kwa ajili ya kujadili masuala ya demokrasia ya vyama vingi, ikiwamo ule ulioitishwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD).

Alisema alisema maazimio ya kumsimamisha Mbatia ni halali kwa kuwa akidi ya wajumbe wake ilikidhi matakwa ya kisheria waliohudhuria walikuwa 52 kati ya wajumbe 82.

**MBATIA AFUNGUKA**

Baada ya kutangazwa kwa taarifa hiyo, Mbatia alisema hatambui mkutano uliofanyika wa halmashauri kuu wa kumsimamisha na kusisitiza kwamba kikao hicho ni batili.

Alisema hakuna kikao kilichofanyika na kwamba atamshangaa Msajili wa Vyama vya Siasa endapo atabariki maazimio ya mkutano huo, akisema anajadiliana na wanachama wenzake kuona hatua za kuchukua.

Mbatia alisema juzi waliwasilisha taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuhusu kikao cha kamati kuu kusogeza mbele mkutano na kuweleza wamemsimamisha kazi Katibu Mkuu wa chama hicho, Matha Chiumba.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama cha NCCR- Mageuzi, Edward Simbeye, alisema kikao kilichofanyika cha kumsimamisha Mbatia siyo cha kihalali na kwamba watakwenda kupambana na Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kuwa ndiye adui wao namba moja katika mgogoro huo.

Simbeye alisema vyama vyote vinaendeshwa kwa mujibu wa katiba na kwamba wajumbe hao hawakuwa na mamlaka ya kumsimamisha Mbatia na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho.

Simbeye alisema watu hao pia hawana mamlaka ya kikatiba, ndiyo maana hawaonekani ofisini, huku akiwaita ni wahuni.

"Watanzania na wanachama wa NCCR-Mageuzi popote walipo nchini leo hatukuwa na kikao cha Halmashauri Kuu kilichofanyika Kurasini ambacho kimeongozwa na Joseph Selasini

"Ni uhaini ndani ya chama na uhuni ambao sisi wanachama vijana, wazee wapenda demokrasia katika taifa letu hatuwezi kukubali uhuni uliofanyika,"alisema Simbeye

Alisema kutokana na kilichotokea hawawezi kuuvumilia na kwamba chama kitakaa katika utaratibu ambao unafaa wa vikao na kufanya maamuzi. Alisema chama cha NCCR-Mageuzi ni chama cha Watanzania, kimesajiliwa kwa mujibu wa katiba na yoyote ambaye wataona anavunja katiba ya nchi hawako radhi kumuona akiendelea kubaki kwenye ofisi ya umma.

Simbeye alisema aliyeitwa Katibu Mkuu wa chama alisimamishwa kujibu tuhuma zinazomkabili Mei 15, mwaka huu katika kikao cha kamati kuu. "Kikao cha Halmashauri Kuu kinaendeshwa na Selasini na kuvunja bodi ya wadhamini Are they sure? Unaweza kuvunja bodi ya wadhamini kihuni huni na kumsimamisha mwenyekiti wa chama huo uhuni hatuwezi kuukubali chama chetu kipo imara,"alisema Simbeye.

Alisema NCCR-Mageuzi kina uzoefu wa kupambana na migogoro ya aina hiyo, hakuna ambaye ataweza kukiua chama hicho, kwamba atakayedhubutu kufanya hivyo Mwenyezi Mungu anaweza kumchukua yeye kabla ya kukichukua chama hicho.

**KAULI YA MSAJILI**

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Sisty Nyahoza, alisema ofisi yake ni mlezi wa vyama vya siasa vyenye usajili kamili na wanavilea kwa mujibu wa sheria ya vyama vya siasa.

Alisema hata wiki iliyopita alikuwa kwenye mkutano wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ofisi ya msajili ilialikwa kwa sababu walikuwa na mchakato wa kuwateua wajumbe wa bodi ya wadhamini.

Kisheria, alisema chama kinavyofanya mabadiliko katika bodi ya wadhamini lazima kuwapo na ofisa wa serikali kwa ajili ya kutazama mchakato huo, kwamba wadhamini wanateuliwa kwa mujibu wa katiba.

Nyahoza alisema kwa upande wao wameshuhudia yaliyotokea wanasubiri taarifa rasmi waipokee kutoka NCCR-Mageuzi ndipo watatoa msimamo.

# Ugonjwa wa fistula bado tatizo nchini

**Na Yasmine Protace**

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, amesema ugonjwa wa fistula ya uzazi bado ni tatizo nchini na kwamba zaidi ya watu milioni mbili duniani wanaishi na ugonjwa huo.

Amesema mbali na idadi hiyo pia kuna visa takribani laki moja vilivyoripotiwa duniani kuwa na ugonjwa huo.

Dk. Mfaume aliyasema hayo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Fistula. Maadhimisho hayo yalifanyika Hospitali ya CCBRT, Jijini Dar es Salaam, kwamba alikuwa mgeni rasmi akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala.

Kutokana na tatizo hilo, Dk. Mfaume alisema elimu inapaswa kuendelea kutolewa na kwamba ugonjwa huo umekuwa ukiwatesa watu ambao wamekuwa wakichelewa kupata matibabu.

Aliipongeza Hospitali ya CCBRT kwa kutoa matibabu bure kwa wagonjwa wa fistula ikiwamo kuwapatia chakula na nauli za kuwatoa mikoani na kuwaleta katika hospitali yao ili wapate matibabu. Mkurugenzi Mtendaji wa CCBRT, Brenda Msangi, alisema ugonjwa wa fistula unatibika, hivyo jamii inapokuwa na wagonjwa hao wawapeleke hospitalini kupata matibabu.

Alisema kesho Tanzania itaungana na huungana na nchi zingine duniani kuadhimisha siku ya kimataifa ya kutokomeza fistula ya uzazi.

"Huu ni mwaka wa 10 tangu tulipoanza kuungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku hii mwaka 2013," alisema.

Msangi alisema kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ni "Tokomeza Fistula, Wekeza, Imarisha Huduma za Afya na Wezesha Jamii'.

Aliongeza kuwa kaulimbiu hiyo inamaanisha kuwekeza na kuimarisha huduma za afya.

Alisema CCBRT ikishirikiana na wadau mbalimbali, ikiwamo serikali, wametekeleza kaulimbiu hiyo kwa kufanya uwekezaji mkubwa kwa kujenga kitengo kipya cha afya ya mama na mtoto ambacho kinalenga kuwahudumia kinamama wenye historia ya fistula.

Msangi pia alisema huwaudumia watu wenye ulemavu, mabinti wanaopata mimba za ututoni, lengo ni kuzuia fistula mpya, pamoja na kuondoa vifo vya mama na mtoto.

Aliongeza kuwa tangu kuanza kwa mapambano dhidi ya fistula mwaka 2003, wamepiga hatua kitaifa katika kutoa matibabu ya fistula kwa maelfu ya kinamama wenye tatizo hilo, kwamba zaidi ya kinamama 17,500 wamepatiwa matibabu hospitalini hapo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Taasisi ya Mwanamke Initiative Foundation (MIF), Fatma Mwasa (aliyevaa koti jeusi), kwa kushirikiana na Taasisi ya Karibu Tanzania, Organization (KTO), wakiwa katika picha ya pamoja na wanachuo wapya 18 kutoka Zanzibar waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi kilichopo Kisarawe mkoani Pwani juzi , baada ya kuwakabidhi msaada wa mahitaji mbalimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sweden yatoa bil.20/- kuendeleza ubunifu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI ya Sweden kupitia shirika lake la maendeleo (SIDA) limetoa zaidi ya Sh. bilioni 20 kwa ajili ya kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu nchini walioshinda katika mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya washindi 83 wa mashindano ya ubunifu yaliyoandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

Kipanga alisema serikali pia imetenga zaidi ya Sh. milioni 700 kwa ajili ya kuendeleza bunifu za wabunifu walioshinda katika mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu yaliyofikia jijini Dodoma.

Alisema fedha hizo zimetolewa na wafadhili hao kwa lengo la kuendeleza ubunifu kwa washindi wa mashindano hayo.

"Tunashukuru wenzetu wa SIDA wametuunga mkono katika mashindano haya, tulikutana nao kuzungumza wakakubali kutuunga mkono ndani ya kipindi cha miaka mitano,"alisema Kipanga.

Akizungumza kuhusiana na fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuendeleza bunifu zilizoshinda, Kipanga alisema fedha hizo zitatumika ipasavyo ili kuhakikisha bunifu zinaendelezwa na kuingizwa sokoni na ziweze kutatua kero zilizopo kwenye jamii.

Alisema hayo ni moja ya maagizo ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliyeagiza kazi za wabunifu walioshinda kuhakikisha zinaendelezwa na kuingia sokoni ili ziweze kulinufaisha taifa na wabunifu wenyewe.

Alisisitiza kuwa katika Bajeti ya Wizara ya mwaka 2020/23 watawekeza Sh. bilioni tisa kutoka Sh. bilioni tatu ambazo zilitengwa kwa ajili ya wabunifu mwaka 2021/2022.

Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, alisema lengo la mafunzo hayo kwa wabunifu ni pamoja na kuwajengea uwezo.

Alisema wanafanya hivyo ili wabunifu waweze kubadilishana mawazo lakini pia kuangalia namna gani hizi wataziendeleza baada ya mafunzo.

Dk. Nungu alisema katika Sh.milioni 700 ambazo zimetengwa kuendeleza ubunifu, Sh. milioni 250 zitatumika kumwendeleza mbunifu wa mita ya maji aliyeshinda mwaka juzi katika mashindano hayo, huku Sh. milioni 500 zitatumika kuendeleza bunifu zilizoshinda mashindano ya mwaka huu.

# Chanzo siri ofisi kuvuja chatajwa

**Na Beatrice Shayo**

MWENYEKITI wa Chama cha Makatibu Mahsusi Tanzania (TAPSEA), Zuhura Maganga, amesema uvujaji wa siri katika sekta yao unasababishwa na taasisi husika kutokuwa na mikakati mizuri waliyojiwekea.

Maganga aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na mkutano mkuu wa TAPSEA unaotarajia kufanyika Juni 2, mwaka huu, mkoani Dodoma mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Ukikuta mahali siri zimevuja ni tatizo la hiyo taasisi kwa kiapo tunachokipata ni wajibu wetu makatibu mahsusi kutunza siri," alisema.

Alisema serikali kwa kipindi kirefu inakemea kwa kuhakikisha watumishi wa umma wanakuwa na maadili na katika utendaji wao wa kazi kikubwa kinachozingatiwa ni uvujaji wa siri.

"Kwa upande wa makatibu mahsusi suala la uvujishaji siri kwa sasa halipo kwa sababu tunasoma katika vyuo vya serikali kikubwa wanachofundisha wanasisitiza utunzaji wa siri katika ofisi," alisema.

Aliongezea kuwa: "Hilo ndilo somo kubwa tunalofundishwa ni lazima kutunza siri hakuna uvujishaji. Tuna kula kiapo na kufuatiliwa na wasimamizi ofisini kujua maadili ya watumishi wake."

Maganga alisema kero wanayokutana nayo ni baadhi ya wateja ambao hufika ofisini kwa ajili ya kupata huduma wanapotaka kwenda kwa bosi akiwauliza shida yao wanakuwa hawataki kueleza.

"Anakuja mgeni anataka kumuona bosi ukimuuliza una shida gani ya kuongea na bosi mara nyingi wanatuona kama tunataka kujua siri zao. Siyo kweli kama tunataka kujua siri kuliko nikupeleke kwa bosi alafu nikaambiwa tatizo lako nikupeleke kwa ofisa fulani huoni kama ungenijulisha tangu awali ungeshahudumiwa tatizo lako kuliko kwenda mpaka kwa bosi," alisema Maganga.

Maganga alisema kazi yao ni kuwasikiliza wageni na kuhakikisha wunapata huduma stahiki kwa wakati na siyo mwananchi kufanya siri katika ofisi za serikali.

Alisema katika mkutano huo ambao unatarajiwa kuanza Mei 31 hadi Juni 3 mwaka huu watashiriki watu 4,000 na zitatolewa mada mbalimbali ikiwamo utunzaji wa siri wakifundishwa na wabobezi kutoka serikalini.

# Waandaa mwongozo kuzuia ndoa utotoni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKOA wa Shinyanga umeanza kuandaa muongozo ambao utatumika kutunga sheria ndogo itakayotathimini ufungaji wa ndoa, lengo kuu likiwa ni kuzuia ndoa za utotoni.

Mratibu wa mpango mkakati wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto mkoani Shinyanga, Tedson Ngwale, alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha kujadili muongozo wa utungwaji wa sheria ndogo kuanzia ngazi za chini, ambazo zitasaidia kutokomeza tatizo la ndoa za utotoni.

Ngwale alisema katika mpango mkakati huo kuna kipengele kinazungumzia utungwaji wa sheria ndogo ili kutokomeza tatizo la ndoa za utotoni.

"Utungwaji wa sheria hizi ndogo utatusaidia kudhibiti tatizo la ndoa za utotoni, sababu kabla ya ndoa kufungwa kutakuwa na fomu ya kujaza ambayo itakuwa kwenye ofisi za watendaji, pia kutakuwa na tathimini ya kujiridhisha kama ndoa hiyo hafungishwi mtoto,"alisema Ngwale.

Aliongeza: "Tunataka hadi kufikia mwaka 2025 ndoa za utotoni mkoani Shinyanga zisiwapo kabisa na kubaki kuwa historia."

Naye Katibu Tawala Msaidizi mkoani Shinyanga, Simbani Liganga, alisema kufanya tathimini ya ndoa kabla ya kufungwa kutasaidia kwa kiasi kikubwa kutokomeza ndoa za utotoni, ambazo hukiuka haki za watoto kwa mujibu wa Sheria namba 21 ya Mtoto ya mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019 na Sera ya Mtoto ya mwaka 2008.

Akizungumzia kuhusu Mradi wa Shirika la Doctors with Africa ambao unalenga kuboresha afya na ustawi wa vijana wa rika balehe, alisema anaimani mradi huo utakuwa ni sehemu ya kudhibiti maambukizi mapya ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) yanayotokana na ukatili wa kingono.

Katika hatua nyingine aliwataka wazazi mkoani Shinyanga kutowaachia jukumu la malezi wafanyakazi wa ndani, ndugu, marafiki, majirani na walimu, ili kutosababisha mmomonyoko wa maadili kwa watoto wao, kufanyiwa vitendo vya ukatili ambavyo huwaathiri kisaikolojia, kimwili na kiafya.

Pia, aliwataka wazazi kuwa na tabia ya kuwakagua miili watoto wao, wanapogundua wamefanyiwa vitendo vya ukatili wachukue hatua na siyo kufumbia macho vitendo hivyo.



Wananchi wa eneo la Kinondo – Mabwepande, Dar es Salaam, wakimsikiliza Meneja wa Mkoa wa kihuduma wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) Mabwepande, Haruna Taratibu (kulia), alipozungumza nao juzi kuhusu mradi wa maji kutoka Makongo mpaka Bagamoyo ambao umewanufaisha wananchi hao. Mradi umefadhiliwa na Benki ya Dunia na kutekelezwa na (DAWASA) kwa bilioni 65.4. PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE

# Hofu yatanda ng'ombe kuchinjwa kwa misumeno

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

Wananchi wa Manispaa ya Songea, wamekumbwa na hofu kuhusu usalama wa nyama wanayokula baada ya kuwapo madai kuwa ng'ombe katika machinjio ya Shule ya Tanga, wanachinjwa kwa kutumia misumeno.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea, Dk. Francis Sagamiko, amewaondoa hofu wakazi wa manispaa hiyo akisema sikweli kwamba mifugo katika machinjio ya Shule ya Tanga inachinjwa kwa kutumia misumeno ya kupasulia mbao.

Akizungumza na Nipashe, Dk. Sagamiko alisema mfumo unaotumika katika machinjio hayo ni wa kisasa na kwamba unafanyakazi vizuri.

Mkurugenzi huyo aliwatoa hofu wananchi kuwa nyama zinazotoka katika machinjio hiyo ni halali ni tofauti na taarifa zilizo zagaa ambazo zimeonyesha kutaka kuichafua serikali.

Juzi, Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Songea likiongozwa na Meya, Michael Mbano, baadhi ya madiwani walisema mashine za kuchinjia nyama katika machinjio ya Shule ya Tanga hazifanyi kazi na badala yake wamekuwa wakitumia mashine za kupasulia mbao kuchinjia mifugo.

Hali hiyo ilisababisha taharuki kwa wakazi wa Manispaa ya Songea. Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakazi wa mji wa Songea walidai kuwa kwa muda mrefu tangu machinjio hiyo ijengwe na kuanza kazi wamekuwa wakiamini kuwa wanyama wanaochinjwa kwenye machinjio hiyo wanachinjwa kitaalamu kwa kutumia mitambo ya kisasa iliyopo kwenye machinjio hiyo.

Walisema wameshtushwa na taarifa zilizotolewa na madiwani kwamba mifugo katika machinjio hiyo imekuwa ikichinjwa kwa kutumia misumeno ya kupasulia mbao. Stephan Komba, Mkazi wa Bombambili Manispaa ya Songea, aliomba serikali kupitia Mkuu wa Wilaya kuchukua hatua za haraka ili kuona namna ya kumaliza matatizo yaliyopo kwenye machinjio hiyo.

Hussein Ngonyani, Mkazi wa Mshangano katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea alisema taarifa aliyoisikia kupitia vyombo vya habari kuhusu machinjio hayo imemsikitisha.

Akizungumza na Nipashe, Dk. Sagamiko alisema: "Siyo kweli kwamba mifugo inachinjwa kwa kutumia misumeno, niwatoe hofu wananchi kwamba nyama inachinjwa kitaalamu na mitambo ya kisasa."

Msimamizi mkuu wa wafanyabiashara ya maduka ya nyama ya ng'ombe, Andrea Kanuda, alisema taarifa hizo si za kweli, na kwamba machinjio hayo yanatumika kila siku wanachinjwa ng'ombe kwa kutumia mashine za kisasa.

Kanuda alifafanua kuwa mashine zilizopo kwenye machinjio hiyo kwa siku wanachinja ng'ombe kati ya 30 hadi 40 na inategemea na hali ya biashara.

Alisema kuwa wanyama wanachinjwa kwenye machinjio hiyo na Shekhe Issa Chamaja aliyeteuliwa na Baraza la Waislam Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Ruvuma, kwamba siyo kweli wananchi wanalishwa vibudu.

Msimamizi mkuu wa machinjio ya wanyama, Said Sangija, alisema kwa wastani zaidi ya ng'ombe 40 wanachinjwa kwa siku katika machinjio hayo.

Alisema matatizo yanayotokea katika machinjio hiyo ni ya kawaida na yamekuwa yakitatuliwa.

Diwani wa kata hiyo, Agaton Goliama, alisema taarifa za mifugo kuchinjwa kwa misumeno ya kupasulia mbao siyo za kweli na kwamba zilikuwa na lengo baya.

# Waziri ataka kukamilika anwani za makazi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo Mathew, amewaagiza watendaji wa Mkoa wa Morogoro kuongeza juhudi katika kukamilisha mchakato wa anwani za makazi.

Alitoa agizo hilo mkoani hapa alipokutana na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Morogoro wakiongozwa Mkuu wa mkoa huo, Martine Shigela, baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa anwani za makazi.

Alisema, Mkoa wa Morogoro umefanya vizuri kwa asilimia zaidi ya 100 katika utekelezaji wa uingizaji wa anwani kwenye mfumo, uanishaji wa barabara, utengenezaji na usimikaji wa nguzo na mbawa zake.

Mhandisi Kundo alisema, mkoa huo haujafanya vizuri katika uandikaji wa namba za nyumba kwani hadi kufikia Mei 16, mwaka huu umefikia ulikuwa asilimia 43.7.

Alisema hatua inayofuata ni kila mwanachi anatakiwa kuwa na anwani za makazi na kwa wafanyabiashara hicho kitakuwa ni moja ya vigezo muhimu katika kuwapatia leseni za biashara.

Mratibu wa anwani za makazi Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Hezron Kilamhama, alisema hadi kufikia Mei 16, mwaka huu kati ya namba za nyumba 609,070 zilizohitajika kuandikwa , nyumba 265,933 tayari zimeandikwa sawa na asilimia 43.7 .

Alisema ukusanyaji na ungizaji wa taarifa za majengo, barabara na anwani za makazi katika mfumo wa TEHAMA unaendelea vizuri na tayari mkoa umefikia asilimia 108.2.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela alisema mchakato wa anwani za makazi umekuwa na ushirikishwaji mkubwa kutoka kada mbalimbali.

## DC ateketeza zana haramu za mil. 173/-

**Na Lilian Lugakingira**, MULEBA

MKUU wa Wilaya ya Muleba mkoani Kagera, Toba Nguvila, ameteketeza zana haramu za uvuvi zilizosalimishwa na wananchi, zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 137.3.

Kusalimishwa kwa zana hizo kumetokana na agizo lake, alilolitoa wiki iliyopita akiwa katika ziara ya kudhibiti uvuvi haramu katika wilaya hiyo, akiwataka watu wote wanaomiliki zana haramu za uvuvi kuzisalimisha ndani ya wiki moja

Nguvila alisema hawezi kukubali vitendo vya uvuvi haramu kuendelea katika wilaya yake na kuwataka wananchi ambao bado wanamiliki zana hizo kuendelea kuzisalimisha kabla ya kukamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

"Tumefanya hili zoezi katika kata saba, tumeangamiza zana haramu katika Kata ya Nyakabango, Kimwani, Rulanda, Gwanseli, Izigo, Katoke na Kata ya Mayondwe ndiyo ya mwisho kwa leo, tutaendelea katika kata zote," alisema Nguvila.

Aidha, Nguvila alimsimamisha kazi Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi wa Rasirimali za Ziwa (BMU) katika Mwalo wa Nyakigera, Charles Magadula, baada ya kubainika kushirikiana na wavuvi kufanya vitendo vya uvuvi haramu katika Ziwa Victoria kwa kutumia makokoro. "Wamiliki wa haya makokoro matatu, moja ni la Veda, mwingine ni Maisha na watatu ni Bahati ambaye kokoro lake wanamiliki kwa pamoja na Mwenyekiti wa BMU, Charles Magadula, nilishamuonya mwenyekiti huyu lakini hakunielewa, sasa kuanzia leo siyo mwenyekiti tena wa MBU, Ofisa Uvuvi tutachagua mwenyekiti mwingine na siyo huyu" alisema Nguvila.

Kaimu Ofisa Uvuvi katika wilaya hiyo, Ignatio Lwinwa, aliwataka wananchi na wadau wa uvuvi, kutoa ushirikiano na kumuunga mkono Mkuu wa Wilaya ya Muleba katika kupambana na vitendo vya uvuvi haramu ili kuhakikisha vinatokomezwa.

Baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe waliishauri serikali kukomesha vitendo vya uvuvi haramu maana vinachangia kurudisha nyuma maendeleo yao kiuchumi, kutokana na kuvua samaki wachanga na kusababisha kupungua ziwani.

# TAKUKURU mguu sawa wadokozi fedha Amcos

**Na Daniel Limbe**, CHATO

WAKATI msimu wa ununuzi wa pamba ukiwa umefunguliwa, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani Chato mkoani Geita imesema imejiandaa vyema kufuatilia vitendo vyote vya rushwa kwa viongozi wa Amcos.

Pia, imewaonya viongozi wa Amcos 53 zinazounda Chama Kikuu cha Ushirika wa Mazao cha "Chato Co-Operative Union (CCU) kutojihusisha na wizi wa pembejeo za wakulima pamoja na fedha za ushirika huo.

Kauli hiyo ilitolewa na Kaimu Kamanda wa TAKUKURU Wilaya ya Chato, Felix Vedastus, kwa wajumbe zaidi ya 100 ambao walishiriki mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi wa Ushirika wa CCU.

Hatua hiyo imekuja baada ya Mrajisi Msadizi wa Ushirika Mkoa wa Geita, Doreen Mwanri, kuzilalamikia baadhi ya Amcos ambazo zimekuwa zikipata hasara kila msimu, huku baadhi ya wajumbe wakidaiwa kuiba pembejeo za wakulima.

Katika mkutano huo, Mwanri alisema serikali haitawaonea huruma baadhi ya makatibu wa Amcos ambao watabainika kujihusisha na wizi wa fedha za ununuzi wa zao la pamba, kwa kuwa hali hiyo isipodhibitiwa inaweza kufifisha jitihada za serikali kuinua ushirika nchini.

"Lazima mtambue kuwa fedha zinazoletwa kwenu kununua pamba ni mkopo na mnapaswa kuzirejesha kwa mujibu wa sharia haiwezekani makatibu wachache watuharibie ushirika wetu kwa tamaa zao binafsi hatutakubali,"alisema.

Alisisitiza kuwapo umoja miongoni mwa wajumbe na viongozi na kujiepusha na vitendo vya kuhujumu ushirika huo kwa kuwauzia pamba safi kampuni za watu binafsi badala ya CCU, ambacho ndiyo chama kikuu cha ushirika huo.

Ofisa Ushirika Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dodoma, Tatu Mwenda, aliwatangaza viongozi wapya wa CCU, kuwa Mwenyekiti ni Gereon Chandika, na Makamu Mwenyekiti ni Emmanuel Ndalahwa.

Wajumbe wa Bodi ya CCU ni Juma Juzenza, Bulamile Katwale pamoja na Kulwa Lukuba ambao wataongoza ushirika huo kwa kipindi cha miaka mitatu.

Aidha Mwenda, aliwataka viongozi waliomaliza muda wao kushirikiana na uongozi huo mpya ili kuinua uchumi wa wakulima wa pamba mkoani Geita pamoja na Kagera.




Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Rashid Mfaume, akijiandaa kumlisha keki mmoja wa wagonjwa wanaotibiwa katika Hospitali ya CCBRT katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Fistula yaliyofanyika kimkoa hospitalini hapo juzi. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Brenda Msangi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NGO zatakiwa kujielekeza kwenye mahitaji

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

TAASISI zisizo za kiserikali (NGO), zimetakiwa kuhakikisha malengo yao yanaendana na vipaumbele na mahitaji ya Taifa.

Wito huo ulitolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula, wakati akifungua mkutano wa wadau wa mashirika hayo uliolenga kukusanya maoni kuhusu mkakati wa kitaifa wa uendelevu wa NGO Kanda ya Kati.

Alisema malengo yao yanapaswa kuzingatia mahitaji ya jamii na mipango iliyopo kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo.

"Serikali inaendelea kuratibu mashirika yasiyo ya kiserikali ili yaweze kufanya kazi zake kwa kuzingatia sheria kanuni na taratibu zilizopo ili kuwahudumia wananchi na miradi wanayotekeleza ilete manufaa na faida kwa wananchi hasa waliopo katika ngazi ya vijiji,"alisema. Pia, aliyataka mashirika hayo kutoa maoni katika kuboresha mkakati wa kitaifa wa uendelevu wa NGOs nchini ili kuwa na mkakati bora ambao utazisaidia kujiendesha na kutekeleza miradi bila wafadhili. "Shabaha ya serikali ni kuhakikisha mashirika haya yanafanya kazi katika mazingira mazuri na kuhakikisha yanachangia katika kuchochea uchumi wa nchi na kuleta ustawi wa jamii,"alisema.

Msajili wa NGO, Vickness Mayao, alisema mashirika hayo yanachangia uchumi wa nchi kutokana na miradi mbalimbali ya maendeleo wanayoifanya.

Alisema taarifa ya mchango wa NGO ya mwaka 2021 inaonesha ajira zaidi ya 8,000 zilitolewa na mashirika hayo katika kipindi cha mwaka mmoja (2020/21).

Mwenyekiti wa kikosi kazi cha kukusanya maoni kuhusu uendelevu wa NGO, Nensia Mahenge, alisema katika ukusanyaji wa maoni ya mkakati wa uendelevu wa NGO imewapa picha kuwa mashirika yapo katika makundi mbalimbali, ikiwamo yale yanayoanza kufanya kazi yanayotegemea ufadhili.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Rais Samia kwa kuwapa ukweli wabunge

**WIKI** hii, Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa na ziara ya kikazi katika mkoa wa Tabora ambako pamoja na mambo mengine alizindua ujenzi wa barabara ya Tabora - Mpanda yenye urefu wa kilomita 342 itakayogharimu Sh. bilioni 473.95.

Baada ya kutekeleza masuala kadhaa ya kiserikali kama yalivyokuwa yamepangwa katika ratiba, Rais alifanya mkutano wa hadhara mjini Tabora ikiwa ni hitimisho la ziara yake hiyo. Moja ya mambo aliyoyazungumza ni juu ya wabunge akiwataka wawajibike katika majimbo yao, ikiwamo kuwahimiza wafanyabiashara kulipa kodi.

Katika hotuba yake hiyo, Rais Samia alisema wabunge wanapaswa kufanya kazi ili kufanikisha kupatikana kwa mapato ya serikali katika mfuko mkuu na hatimaye kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Alisema bila kufanya hivyo, serikali haiwezi kupata mapato kwa ajili ya maendeleo hatua ambayo itarudisha nyuma maendeleo ya sekta mbalimbali.

Bila kumung'unya maneno, Rais alisema wabunge wamekuwa na tabia ya kudai kutekelezewa masuala mbalimbali ya maendeleo kama vile elimu, afya na barabara katika maeneo yao ilhali hawawajibiki kuhimiza maendeleo ikiwamo kuwataka wafanyabiashara kulipa kodi kwa mujibu wa sheria.

Tabia hiyo ya wabunge kudai mambo mbalimbali imekuwa ikijitokeza katika ziara za viongozi wakuu wa serikali wakiwamo Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwenye mikoa yao hususan wanapofika kwenye wilaya.

Kila mara wabunge hao wamekuwa wakitumia majukwaa hayo kuomba mambo mbalimbali. Sambanba na ziara za viongozi wakuu, hata michango yao katika bunge, ikiwamo ile ya mijadala ya bajeti na makadirio ya mapato na matumizi ya serikali imekuwa vivyo hivyo.

Baada ya baadhi ya wabunge wa mkoa wa Tabora, akiwamo aliyekuwa waziri katika serikali iliyopita, Joseph Kakunda, kuomba mambo mbalimbali kutoka kwa Rais kwa ajili ya jimbo lake, hatimaye Rais alitoboa ukweli kuwa hakuna haki bila wajibu. Maana yake ni kwamba kabla ya kuomba mambo hayo, lazima watimize wajibu wao wa kuhimiza wafanyabiashara katika maeno yao kwa ajili ya kulipa kodi.


Hakika kwa jambo hilo, Rais Samia amewafungua macho Watanzania kwamba hakuna haki bila wajibu kwa maana kwamba mtu lazima awajibike kwanza kabla ya kudai ujira na huo ndio mfumo halisi wa maisha ya kawaida.

Ni wakati sasa wabunge wetu na viongozi wengine waliochaguliwa kwa ajili ya kuwakilisha wananchi katika ngazi mbalimbali za uamuzi, kuchukulia kauli ya Rais kama changamoto kwao. Wanachopaswa kujiuliza ni mambo gani wamewajibika kabla ya kudai haki. Kwa maneno mengine, kabla ya kulalamikia kero zilizoko katika maeneo yao, kwa maana ya kata na majimbo, wanapaswa kujiuliza ni namna gani wamezishughulikia kabla ya kuziwasilisha mbele baada ya kujiridhisha kwamba wameshindwa.

Wabunge ni wawakilishi wa wananchi, hivyo kabla ya kuwasilisha kero zinazowakabili wananchi wao ngazi za juu, wanatakiwa kutafuta namna ya kuzitatua kwa kushirikiana na wananchi wao. Si kila kitu ni lazima kipelekwe kwa viongozi wakuu wa serikali.

Ni wakati wa wabunge na wawakilishi wengine wa wananchi kuamka na kuanza kuwajibika katika kuhimiza masuala ya maendeleo badala ya kuonekana ni mabingwa wa kutoa hoja mbele ya viongozi. Wajiulize wamefanya nini kabla ya kufanya hivyo?

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hujuma hizi zinakwamisha maendeleo ya nchi

Na Sabato Kasika

**RAIS** Samia Suluhu Hassan ameonyesha kukerwa na wizi wa miundombinu ya barabara unaofanywa na baadhi ya watu na kusema wanaofanya vitendo hivyo ni wahujumu uchumi, wanatakiwa kuchukuliwa hatua za kisheria.

Ni wakati akizindua barabara mpya mkoani Tabora wiki hii na kufafanua kuwa miundombinu hiyo ambayo serikali inajenga kwa gharama kubwa ni kwa manufaa yao lakini anashangaa kuona baadhi ya watu wakiihujumu.

Baadhi ya miundombinu inayodaiwa kuibwa ni taa za barabarani na nguzo, huku Rais akiagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kuwatafuta wote waliohusika kuhujumu miundombinu ya barabara ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Kimsingi, hujuma hizo zinaonyesha ni jinsi gani baadhi ya Watanzania wasivyothamini wala kutunza vitu vyao ambavyo serikali inavifanya kwa manufaa yao na tena kwa kutumia fedha zao wenyewe.

Kwa mfano, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila, anasema ujenzi wa barabara ya Nyahua hadi Chaya umehusisha madaraja makubwa mawili na makalvati makubwa 32.

Vilevile kuna makalvati madogo 60, na kwamba ujenzi huo umegharimu zaidi ya Sh.bilioni 123 kutoka serikali ya Tanzania ambazo ni kodi ya wananchi na Mfuko wa Maendeleo ya Kiuchumi wa Kuwait.

Inashangaza kuona baadhi ya watu wakifanya hujuma kwenye miundombinu ambayo imejengwa kwa fedha zao wenyewe kupitia kodi. Ninadhani watu wa aina hiyo wanatakiwa kusaidiwa kuachana na mtindo huo.

Ninadhani ipo haja wananchi kuelimishwa umuhimu wa kulinda miundombinu, kupitia vyombo vya habari wajue kuwa wanatakiwa kutoa taarifa kwa mamalaka husika wanapoona kuna hujuma au viashiria vya hujuma.

Usimamizi wa miundombinu inayojengwa kwa manufaa ya umma, upo chini ya umma wenyewe, hivyo iwapo akijitokeza mtu na kuiharibu, umma hauna budi kumchukulia hatua ikiwamo kumfikisha kwenye vyombo vya sheria.

Sidhani kama ni sahihi kuona mtu akiiba taa ya barabara, sola au vitu vingine ambavyo vimewekwa kwa ajili ya uimara wa barabara halafu akaachwa aendelee kufanya hujuma bila kumchukulia hatua.

Ninaona kuwa huu siyo wakati wa kuendekeza msemo usemao; 'mali ya umma haina mwenyewe', msemo huo ukiendelea kupewa nafasi, basi hujuma za miundombinu zitazidi kuongezeka na kukwamisha maendeleo.

Suala la utunzaji wa miundombinu haliishii kwenye barabara tu bali hata ya maji, umeme na mingine mingi ambayo baadhi yake imekuwa ikihujumiwa na wananchi badala ya kuwa mstari wa mbele kuilinda.

Nitolee mfano miundombinu ya maji, bomba linaweza kutoboka kidogo na kuvujisha maji, badala ya watu kutoa taarifa kwa mamlaka husika ili lizibwe, wao wanaweza wakaongezea kulipasua ili wapate maji mengi.

Mtindo huo si mzuri na unaweza kukwamisha watu wengine kupata huduma hiyo, hivyo ninadhani pamoja na mambo mengine, elimu kwa watu wa aina hiyo inahitajika ili waelewe umuhimu wa kulinda miundombinu.

Kwa ujumla ni kwamba, hujuma kwenye miundombinu ya barabara na maji imekuwa ikifanyika mara kwa mara na tena inafanywa na watu wa maeneo husika bila kujali kuwa ipo kwa manufaa yao.

Ni muhimu kutambua kuwa utunzaji wa miundombinu una pande mbili, ambapo wa kwanza ni serikali ambayo inawajibika moja kwa moja kuwa mtunzaji mkuu huku wananchi nao wakiwa na jukumu hilo pia.

Si vyema wananchi kumuona mtu akifanya hujuma wakamnyamazia, bali wajue kuwa wanatakiwa kumfikisha kwenye vyombo vya sheria na kwa njia hiyo ninaamini hujuma kwenye miundombinu zinaweza kupungua.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Mfano huu uigwe na taasisi kwa kuzijengea uwezo jamii



Na Pascal Mayalla

**Mababu zetu wakapewa gololi nzuri za kupendeza, wakafurahi sana na wao kuzitoa almasi zao zote walizokuwa nao na kuwapa wazungu hao. Kumbe masikini mababu zetu hawakujua wamefanywa mazuzu. Kule kufurahia gololi na kutoa almasi ulikuwa uzuzu kwa sababu walikuwa hawajui.**

KWA Maslahi ya Taifa leo, inazungumzia kitu kinachoitwa kwa lugha ya Kiingereza Corporate Social Responsibility (CSR). Hiki ni kitendo cha kampuni au taasisi kurejesha katika jamii sehemu ya faida inayopata kwa kufanya jambo lolote kuisaidia jamii.

Tanzania tuna kampuni nyingi zinazotengeneza faida za mamilioni kama si mabilioni ya shilingi. Kutokana na faida hizo kuna baadhi ya kampuni hutumia faida hiyo kwa kulipana mishahara minono, huku jamii iliyowazungunguka ikiishi katika hali ya umasikini uliotopea.

Binafsi natoka Kanda ya Ziwa, eneo lililojaliwa utajiri mkubwa wa madini kuanzia almasi, dhahabu na vito. Madini hayo yanapatikana chini ya ardhi na wakazi wa maeneo hayo ndio waliobarikiwa na Mwenyezi Mungu kuyamiliki madini hayo. Kwa maana hiyo ni madini yao lakini kwa vile si tu walikuwa hawajui na hata baada ya kujua, hawawezi kuyachimba kwa sababu hawana ujuzi, zimeingia kampuni kuvuna rasilimali hiyo.

Wakoloni walipokuja nchini, waliwakuta Wasukuma fulani wanatumia mawe ya almasi za mviringo zilizokuwa zinaokotwa mtoni, kuchezea mchezo wa bao. Wazungu hao wakagundua kuwa mawe hayo ni almasi ambayo kwa wakati huo ndiyo madini yenye thamani kubwa kuliko madini yote ya vito. Wakarudi kwao ulaya, wakatengeneza gololi za chupa zenye mviringo mzuri kuliko yale mawe ya mtoni, wakazitia na nakshi za rangi rangi za kupendeza, wakazileta nchini kwetu na kwenda kuwagawia bure wale wazee wa Kisukuma, kwa kubadilishana na zile Almasi walizotumia kuchezea bao.

Mababu zetu wakapewa gololi nzuri za kupendeza, wakafurahi sana na wao kuzitoa almasi zao zote walizokuwa nao na kuwapa wazungu hao.

Kumbe masikini mababu zetu hawakujua wamefanywa mazuzu. Kule kufurahia gololi na kutoa almasi ulikuwa uzuzu kwa sababu walikuwa hawajui.

Baada ya Wakoloni kugundua utajiri huo wa madini ya almasi, wenyeji wa maeneo hayo wakahamishwa, ukajengwa mgodi wa kwanza nchini na mzungu Fred Williamson, eneo la Mwadui mkoani Shinyanga na kuitwa kwa jina lake. Kwa wale waliowahi kufika Mwadui, ukaingia mgodini, ukaona maisha ya wafanyakazi wa mgodi wa Mwadui ukilinganisha na maisha ya wale Wasukuma wenye almasi zao, kama una machozi ya karibu, unaweza kulia.

Hali ni hiyo karibu maeneo yote yenye madini nchini, baada ya kugunduliwa madini, wenyeji huhamishwa eneo hilo na kupewa wawekezaji ambao huliendeleza kwa kujenga kambi zenye miundombinu ya kisasa. Wafanyakazi wa migodini kulipwa vizuri, huishi vizuri kama peponi, huku wenyeji ambao ndio wamiliki halisi wa madini hayo, wakiishi katika maisha ya umasikini uliotopea.

Hali hii ya kampuni kutengeneza faida kubwa, iko kwa makampuni mengi na hata wafanyabishara wengi ambao faida yao inatokana na jamii iliyowazunguka lakini ukilinganisha wanachopata na faida wanayorudisha kwa jamii ni mbingu na nchi!

Ili kuishi vizuri na jamii iliyowazunguka, kampuni hizo zimebuni sera ya CSR ili kurudisha kidogo kwenye jamii. Wakoloni wao walichorudisha kwenye jamii ya wale Wasukuma wa almasi ni gololi lakini kuna kampuni zinarudisha soda, peremende na mlo wa siku moja kwa jamii iliyowazunguka.

Kwa nchi za wenzetu zinazoitwa 'Tiger Nations', wanamsemo "Ukiwakuta watu wamezungukwa na samaki, huku wanalala njaa kwa sababu hawawezi kuvua samaki, usiwavulie samaki na kuwapa mlo wa samaki, wale washibe walale ukitaka kuwasaidia. Badala ya kuwagavia bure samaki, wafundishe kuvua samaki kwa kuwajengea uwezo na kuwapa vifaa".

Nchi hizo sisi Tanzania tulipata nazo uhuru wakati mmoja miaka ya 1960s sisi tukiwa na kila kitu, wenzetu wakiwa hawana kitu. Lakini leo tukijilinganisha nao ni mbingu na nchi.

TotalEnergie ni moja ya kampuni kubwa za mafuta nchini, yenye sera ya CSR ya kulisaidia taifa. Kila mwaka inafanya shindano la kubuni miradi mipya na kutoa Sh. milioni 100 kwa miradi inayoshinda, kuzitumia kujengea uwezo ili miradi hiyo iwe endelevu.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Ali Gugu, aliyekuwa mgeni rasmi katika sherehe za kampuni hiyo kwa mwaka huu, alisema sekta binafsi ndio injini ya uchumi wa taifa, hivyo serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili wajasiriamali wadogo na wa kati nao wakue na kuzalisha kada ya mamilionea na mabilionea wazawa ambao watachangia katika uchumi wa taifa.

Gugu alipongeza TotalEnergies kwa shindano hilo na kutoa zawadi za zaidi ya Sh. milioni 100 na kati ya hizo, washindi watatu wa mwanzo, kila mmoja alipewa hundi ya Sh. milioni 20 kuboresha mitaji yao na kuwalea kwa mwaka mmoja kwa kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo na kuwaangazia fursa za masoko.

Mkurugenzi Mkuu wa TotalEnergies Tanzania, Jean-Francois Schoepp, alisema lengo la TotalEnergies, si tu kufanya biashara na kuzalisha faida bali kuitumia hiyo faida inayopatikana na kuwajengea uwezo na wengine ili kuwainua na kuliinua taifa kiuchumi.

Kama kampuni zingine zote zinafanya biashara Tanzania na kutengeneza faida, badala ya kufanya CSR za kugawa peremende, badala yake zifanye CSR za kujenga uwezo, Tanzania tungekuwa wapi?.

**Wasalaam.**
**Pascal Mayalla**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tulia endelea kutuliza mawaziri wa hivyo



Na Joseph Kulangwa

**'Bibi Mchele' wakati huo, akasema siku zote akitamani naye aingine barazani humo, ili akasaidie kubana mawaziri ili wajibu maswali inavyotakiwa, lakini kubwa waseme ukweli kwa wawakilishi wa wananchi na wao kwa ujumla.**

KUNA mambo unaweza kuyasikia au kuyashuhudia yakakufikirisha sana lakini ndipo unaweza pia kujua hii dunia imeumbwa na ina viumbe wake wanaoifanya iitwe hivyo.

Hivi ukimwamini mtu akufanyie mambo yako ukidhani ndiye hasa anayestahili kuyafanya lakini hatimaye ukajikuta hufanyiwi unavyotarajia, utafikiria umeibiwa au?

Mathalan unajipinda kuchagua kiongozi ukiamini ndiye atakayekusaidia kupambana na matatizo yanayokukabili, lakini akaja kufanya kinyume chake, utafikiria nini?

Watanzania tunaishi katika ulimwengu wa kuongoza na kuongozwa, tunapata viongozi kwa kuchagua na kuteua na wote huapa kutekeleza majukumu yao inavyopasa na tuna utaalamu wa kutambua majukumu yao kwa kuwalipa stahiki zote.

Tuna taasisi mbalimbali ambazo tumezipa watu wenye majukumu ya kusimamia mambo ya kiuwakilishi na kiutawala na wote tunatarajia watimize majukumu yao kikamilifu. Wakifanya kinyume kwa kweli tunakuwa hatuwaelewi.

Tuna chombo au mhimili mkubwa na mzito, wenye manufaa makubwa kwetu. Mhimili huo ni Bunge ambao ndio hugusa moja kwa moja maisha ya watu na ndiyo sababu hupata wawakilishi kwa kuwapigia kura.

Wawakilishi wetu hao huitwa wabunge ambao sisi huwachagua na baadhi yao mkuu wa nchi huwateua kuwa mawaziri, wakimwakilisha au kumsaidia kukidhi mahitaji ya wananchi waliomchagua, hivyo huwekeza fikra na matumaini yake kwao.

Inapotokea wabunge au wawakilishi wa wananchi na wawakilishi wa Rais hawakutimiza majukumu yao ya msingi, huwa ni bahati mbaya sana si kwa wananchi au Rais tu, bali jamii yote kwa ujumla wao.

Hebu fikiria mbunge anakwenda bungeni kusinzia au kama anazungumza kwa kutoka nje ya mstari, yaani badala ya kuzungumzia kadhia zinazowakuta wapigakura wake, anazungumzia mambo yake au anachekesha.

Hao ndio Chifu Hangaya wakati fulani alishindwa kujizuia akasema wanademka bungeni, yaani wanahanikiza mipasho tu na kusahau kuwa wako pale kwa ajili ya kuzungumzia mambo ya wananchi waliowatuma pale.

Fikiria Waziri anaulizwa swali na mbunge naye badala ya kumjibu anachokitaka, anatoka mstarini na kusema ajuavyo yeye, bila kuzingatia kuwa maswali yanalenga kujua nchi inakwendaje au inafanya nini katika kusaidia wananchi.

Hili la Spika, Dk Tulia Ackson, kuwatolea uvivu baadhi ya mawaziri waliodemka badala ya kujibu walichoulizwa, wakasema yao, linafikirisha sana. Na kama asingekuwa macho Spika, hayo yangepita kama yalivyojibiwa kwa kupaswa na mawaziri hao, hivyo wabunge kubaki hawaelewi.

Uamuzi wa kutaka majibu hayo yakaandaliwe upya na kurudiwa kujibiwa siku nyingine ni mwafaka kabisa na inaonesha ni kwa jinsi gani Spika alivyo macho, na anavyofuatilia wawakilishi wa wananchi na wale wa Mkuu wa Nchi.

Inanikumbusha kauli aliyopata kuitoa Chifu Hangaya, wakati akisimulia safari yake ya kufikia kilele cha kuongoza nchi kwamba hapo zamani hakuwa anafurahishwa na majibu ya mawaziri katika Baraza la Wawakilishi.

'Bibi Mchele' wakati huo, akasema siku zote akitamani naye aingine barazani humo, ili akasaidie kubana mawaziri ili wajibu maswali inavyotakiwa, lakini kubwa waseme ukweli kwa wawakilishi wa wananchi na wao kwa ujumla.

Alidhamiria hilo na akagombea uwakilishi, lakini kwa kudra za Mwenyezi Mungu alipofanikiwa kuchaguliwa, akajikuta mbanaji anabanwa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri na badala yake kuwa mjibu maswali badala ya mwuliza maswali.

Alichokifanya Dk. Tulia ni kwamba alipita kwenye nyayo za Chifu Hangaya, ambaye hataki ubabaishaji wa baadhi ya viongozi kwa wananchi. Hivi kwa nini usitekeleze majukumu yaliyokupeleka hapo tena kwa malipo na badala yake udemke?

Hili la Dk. Tulia bila shaka litakuwa shule au darasa kwa mawaziri wengine na hata viongozi wa mitaani, kwamba ukipewa jukumu litekeleze inavyopasa, kwa kutenda yanayotakiwa ili wananchi waendelee kuwa na imani nawe, lakini pia na nchi yao.

Ikumbukwe na kuzingatiwa, kwa viongozi, kwamba mnapokuwa mmepewa dhamana msijisahau mkadhani kuwa waliobaki huku nje hawana uwezo wa kuingia huko mliko na kufanya myafanyayo tena pengine kwa ubora zaidi.

Kitendo cha mawaziri kutakiwa kwenda kuchimba zaidi na kurudi kujibu kwa ufasaha, maswali yaliyokwishaulizwa si tu kunapoteza muda, bali pia rasilimali za Taifa zinachezewa. Tunatarajia utendaji mzuri na uliotukuka kwa viongozi wetu, katika kuwasaidia Spika Tulia na Chifu Hangaya. **Alamsiki!**

# Dk.Mwinyi atambua mchango wa Magoa kwenye maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inathamini mchango wa Jumuiya ya Magoa Zanzibar katika kuendeleza shughuli za maendeleo zikiwamo huduma za kijamii.

Aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar alipofanya mazungumzo na Jumuiya ya Magoa Zanzibar chini ya Mwenyekiti wake, Amanda Demello.

Dk. Mwinyi alisema kuwa Jumuiya ya Magoa Zanzibar kama zilivyo jumuiya nyingine imekuwa na mchango mkubwa katika kuiunga mkono Serikali kupitia shughuli mbalimbali za maendeleo zikiwamo za biashara, huduma za kijamii, uwekezaji na hata sekta ya utalii.

Hivyo, Dk. Mwinyi alisisitiza kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na jumuiya hiyo katika kuhakikisha inatekeleza vyema shughuli zake, zikiwamo huduma zake za kiroho kwa azma ile ile ya kuendeleza amani na utulivu. Dk. Mwinyi alisema ni jukumu la Serikali katika kuwapelekea wananchi huduma muhimu za kijamii, lakini kutokana na uwezo wake kuwa mdogo jumuiya kama hizo zimekuwa zikiiunga mkono Serikali kutoa huduma kwa wananchi jambo ambalo ni la msingi na la kupongezwa.

Dk. Mwinyi alieleza kwamba ujio wa jumuiya hiyo Ikulu na kupata fursa ya kuzungumza mambo mbali mbali ikiwa ni pamoja na kueleza matatizo waliyonayo kunazidi kuleta uhusiano na ushirikiano wa kihistoria uliopo kati ya serikali na jumuiya hiyo.

Akizungumzia suala la uwapo wa mapapasi ambao wamekuwa wakiwasumbua wageni wanaotembelea Mji Mkongwe pamoja na fukwe mbalimbali katika visiwa vya Zanzibar, Dk. Mwinyi alisema juhudi za makusudi zitachukuliwa kupitia kikosi maalum cha Askari wa Utalii katika kuhakikisha mambo kama hayo hayatokei.

Kadhalika, Dk. Mwinyi alitilia mkazo suala la kupewa kipaumbele kwa somo la historia katika skuli za Zanzibar hasa ikizingatiwa kwamba sekta ya utalii ambayo ndiyo sekta muhimu katika uchumi wa Zanzibar inahitaji historia. Hivyo, Dk. Mwinyi alitumia fursa hiyo kueleza juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuupitia upya mfumo mzima wa elimu ya Zanzibar ili iweze kuleta mabadiliko makubwa na kurudi katika hadhi yake kama ilivyokuwa hapo kabla.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Magoa Zanzibar, Amanda Demello alitoa shukrani kwa Dk. Mwinyi kwa kuipa jumuiya hiyo fursa ya kukutana nae na kuweza kubadilishana nae mawazo.

Amanda alisema kwamba Magoa walianza kuingia Zanzibar karne ya 18 kutoka Goa, nchini India kwa kutumia majahazi na meli za abiria.

Aliongeza kuwa katika karne ya 20 Magoa waliongezeka na kuwa wengi zaidi katika visiwa vya Zanzibar, Unguja na Pemba na kushika nyadhifa mbalimbali ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kabla ya mapinduzi na baada ya mapinduzi.

Kadhalika, alitumia fursa hiyo kueleza matatizo yanayokabili jumuiya yao ikiwa ni pamoja na kukosa sehemu ya kukutana pamoja na kufanya shughuli zao kama ilivyo kwa jumuiya kama hiyo kwa upande wa Dar-es-Salaam, Arusha, Nairobi, Tanga na Mombasa.

Alisema Jumuiya ya Magoa walioko Zanzibar ina matumaini makubwa na Serikali anayoiongoza Dk. Mwinyi kwani wanakubaliana na maendeleo yaliyofanyika kwa muda mfupi aliokaa madarakani na wanazikubali juhudi anazozichukua za kimaendeleo na kuwaweka wananchi wote wa Zanzibar kuwa kitu kimoja.



Wafanyakazi wa Machinjio ya Nyama ya Shule ya Tanga Manispaa ya Songea wakimswaga ng'ombe kumwingiza kwenye eneo la kuchinjia jana. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

# Pinda asifu juhudi TFS ufugaji nyuki

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, ameupongeza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa kuhamasisha ufugaji wa nyuki na kuwawezesha wananchi kujiongezea uchumi kupitia mazao yanayotokana na nyuki.

Alitoa pongezi hizo jana alipokuwa akikagua mabanda ya washiriki wa Maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani ambayo kitaifa yalifanyika katika uwanja wa Azimio, Mpanda mkoani Katavi.

Pinda ambaye amekuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo, alisema awali TFS ilikuwa ikihamasisha wananchi kikamilifu namna ya ufugaji nyuki hali iliyokuwa ngumu kueleweka kuliko ilivyo sasa. Alisema kwa sasa TFS inazalisha pia mazao ya nyuki hai itakayowasaidia wananchi kujifunza kwa nadharia na vitendo.

"TFS sasa SAFI! Naona mnazalisha mazao mbalimbali ya nyuki lakini kikubwa nimefurahi kuona mnazalisha chamvua, sasa muwahamasishe wafugaji kuvuna chamvua ili kujiongezea uchumi wa kifedha kwa kuwa zao hili lina thamani kubwa ukilinganisha na asali yenyewe.

"Mmeniambia hapa inawachukua siku saba kuzalisha kilo moja na nusu ya chamvua kutoka kwenye mizinga 20 ambayo kilo hio mnauza kwa Tsh. 300,000 hii ni habari njema, nilizoea kusikia Vumbi la Singida inayozalishwa na Kijiji cha Nyuki Singida sasa na nyie mmechangamkia fursa, sasa mvipe ujuzi huu vikundi mbalimbali vya ufugaji nyuki," alisema Pinda.

Alisema ili kufanikisha ufugaji wa nyuki na kuvuna chamvua, wafugaji wanatakiwa kuunda vikundi mbalimbali vya ufugaji kisha vipatiwe elimu ya namna ya kufuga kwa mfumo wa kisasa na mwisho wa siku wanakuwa wafugaji bora wa wadudu hao ambao hutoa mazao mbalimbali likiwamo zao la chamvua ambalo lina thamani kubwa na soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

Pinda pia alipongeza kazi inayofanywa na TFS kwa kulinda mapori mengi Tanzania na kuyafanya yaendelee kuwa na uoto wa asili jambo ambalo litaongeza uzalishaji wa mazao yanayotokana na nyuki.

Kamishna Msaidizi anayesimamia Rasilimali za Nyuki TFS, Hussein Msuya, alisema wakala umejipanga kuhakikisha elimu inatolewa kwa wafugaji wa nyuki kwa nadharia na vitendo.

Msuya alisema kwa kushirikiana na Wizara kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani, wamezindua kampeni ya kutundika mizinga katika msitu wa Manga mkoani Katavi na mizinga 40 ilitundikwa kwenye eneo hilo.

# Kituo chapunguza gharama watumishi kufuatilia maslahi

**Na Veronica Mwafisi,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amesema, Kituo cha Huduma kwa Mteja cha ofisi yake tangu kianze kutoa huduma, kimewapunguzia gharama watumishi wa umma na wananchi waliokuwa wakilazimika kusafiri umbali mrefu kufuatilia utekelezaji wa masuala yao ya kiutumishi.

Mhagama alisema hayo jana jijini Dodoma, alipofanya ziara ya kikazi katika Idara ya Ukuzaji Maadili iliyoko Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) ili kujionea namna kituo hicho kinavyofanya kazi.

Alisema tangu kituo hicho kianze kutoa huduma rasmi, kumekuwa na faida kubwa katika kuwapunguzia gharama Watanzania wanaofuatilia masuala yao ya kiutumishi na wanaohitaji ufafanuzi wa masuala ya kiutumishi katika ofisi yake. "Watoa huduma katika kituo chetu wamekuwa wakipokea baadhi ya hoja zinazoihusu ofisi yangu na nyingine nyingi zinahusu taasisi zingine za serikali, hivyo ofisi yangu imekuwa ikitoa ufafanuzi na elimu kwa Watanzania ili wawasilishe hoja zao mahali sahihi," alisema.

Mhagama alisisitiza kuwa kituo hicho kimeisaidia ofisi yake kufuatilia mwenendo mzima wa hali na ustawi wa utumishi wa umma nchini, ikiwa ni pamoja na kuwasaidia watumishi wa umma kuwa karibu na ofisi yake iliyopewa dhamana ya kusimamia masuala ya kiutumishi na utawala bora.

Alifafanua kuwa kituo hicho kinatoa huduma siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 10:00 jioni.

"Ukitaka kupata huduma katika kituo chetu tumia namba 0262 160 240 na kila atakayeipata namba hii ampatie na mwingine ili ofisi yangu itoe huduma, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi," alisisitiza.

Kuhusu maadili ya watoa huduma wa kituo hicho, Mhagama alisema watumishi hao wamepatiwa mafunzo ya maadili, hivyo ni waadilifu na wanatoa huduma kwa kuwajali wateja.

Waziri pia alipata fursa ya kutoa huduma kwa watumishi wa umma waliopiga simu katika kituo hicho, hivyo kutatua changamoto za kiutumishi zilizokuwa zikiwakabili watumishi hao.

# MAISHA

MEI 22, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 13

**Mavazi ya mazoezi**



**MAISHA NI NYUMBA**

Kumbe nyumba nazo hukumbwa na fangasi!



Ukurasa 12

**HARUSI**




# Kabiliana na mionzi ya jua

Ukurasa 14


# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | T | E | M | B | O |
| | A | | | A | |
| A | M | A | | B | |
| | B | | T | U | A |
| | U | | | K | |
| M | A | M | B | A | |





## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UDA, UMA, SANDA, TAMKO, KANDIA, TAMBUA

## CHEKA



Alichokifanya Adaktari

MTOTO Asha alikuwa akimchana nywele mama yake, wakati akiendelea kumchana kwa kutumia chanuo ghafla alimchoma kidogo nyuma ya sikio. Mama yake aliguna na kisha alimtazama na kumwambia asitumie nguvu wakati wa kuchana nywele na badala yake atumie akili nyingi.

**Mama:** Umenielewa Asha wakati wa kuchana nywele kuwa mwangalifu ili usiniumize masikio

**Asha:** Sawa mama, lakini mwalimu alituambia eti sikio la kufa halisikii dawa, kwani masikio nayo yanakufa?

**Mama:** Hapana mwanangu, huo ni msemo tu ambao unaelekeza kuwa jambo lolote likifikia mwisho hakuna mtu anayeweza kusaidia.

**SWALI**

Mnyama anayeitwa Kima Punju anapatikana wapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Huwezi kuvuna zaidi ya kile ulichowekeza

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kuchambua kwa nini watu wengi hukata tamaa katika kusaka mafanikio yao. Ziko sababu kadhaa na wiki iliyopita nilitaja mojawapo ambayo ni kutarajia mafanikio ya haraka.***

Nikasema kuna watu wanatarajia kupanda leo na kuvuna kesho, hawana subira. Watu wa aina hii wanashindwa kuelewa kwamba uvumilivu ni tunda la Roho na ni nguzo kuu ya mafanikio ya wanadamu.

Sasa leo tuangalie sababu zingine zinazochangia watu kukata tamaa katika maisha yao. Kutarajia matokeo makubwa kuliko ulivyowekeza ni eneo lingine linalotesa wengi pasipo kujua.

Unapopanda mazao kwenye ekari moja tarajia kuvuna mazao ya ekari moja. Acha kulalamika kwa nini hupigi hatua katika maisha. Tambua kanuni hii kuu, unavuna ulichopanda.

Hata utunze vipi shamba lako kama ni ekari moja litakupa mazao ya ekari moja tu.Ukitaka zaidi panua shamba, yaani wekeza zaidi. Hili ni rahisi kulielewa lakini ni ajabu jinsi wengi wanavyowekeza kidogo na kutarajia kupata vingi, na wasipopata hukata tamaa na kulaumu!

Mungu katika moja ya maandiko yake anasema: " Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba na apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu". Mungu ni wa vingi na anakusudia kukupa vingi kwa sababu amewekeza ndani yako uwezo wa kuongezeka! Hata hivyo hatulazimishi kuongezeka, uamuzi huo upo mikononi mwetu.

Mungu daima anasimamia kanuni zake. Cha ajabu ni kule kumtegemea azivunje kwa ajili yako, yaani unapanda kidogo halafu unamtarajia atende muujiza kwa kukupa zaidi ya kile ulichopanda.

Hapa msomaji wangu nazungumzia ule mtiririko wa mafanikio katika maisha yako kutokana na maono Mungu aliyokupa. Ukitambua kuwa huwezi kuvuna zaidi ya kile ulichopanda utatarajia mavuno au mafanikio yanayolingana na ulivyowekeza. Utambuzi huu utakuwezesha kujipanga vizuri na kujipanua zaidi.

Ukitaka matokeo tofauti, badilisha kile unachofanya. Huwezi kupata unachotaka huku ukiendelea kufanya hicho unachofanya bila kubadilisha. Albert Einstein, mwanasayansi Mjerumani, aliyegundua nguvu ya atomiki aliwahi kusema; "Wazimu ni kule kurudia kufanya jambo lile lile na kutarajia matokeo tofauti".

Sababu nyingine inayofanya watu kukata tamaa ni kutojipanga kwa yasiyotarajiwa. Upo mfano wa mtu mmoja aliyepanda mbegu njema katika shamba lake. Lakini watu walipolala, akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano. Baadaye majani ya ngano yalipomea na kuzaa, tazama yakaonekana magugu!

Mtu huyu japokuwa alipanda mbegu njema lakini alishuhudia magugu asiyoyatarajia. Wengi wetu tunajipanga kufanikiwa bila kuzingatia ukweli kwamba unaweza kukutana na vikwazo usivyotarajia!

Kila mwenye hekima ya Mungu hujipanga akitambua kuwa njiani atakutana na vikwazo katika safari yake kuelekea mafanikio. Katika mfano huo hapo juu, aliyepanda magugu alikuwa ni adui. Yupo mtu mmoja tu ambaye daima husimama kuzuia mafanikio yako, huitwa shetani. Atatumia kila aina ya hila kukufanya ushindwe kujipanga kukabiliana na yasiyotarajiwa!

Wataalamu wa masuala ya miradi na mpango kazi husisitiza kujumlisha kipengele cha yasiyotarajiwa katika utekelezaji wa maono yao. Hujulikana kama "Risk management", au kwa tafsiri ya 'Udhibiti wa yasiyotarajiwa'.

Udhibiti wa yasiyotarajiwa hukupa upeo mpana wa kujipanga vema ili kudhibiti matukio yasiyotarajiwa katika utekelezaji wa malengo yako. Kama unapanga kulima nyanya, kwa mfano, utaanza kwa kuchambua yale yote unayohitaji na ipi iwe njia mbadala kukuepusha na yale yasiyotarajiwa.

Udhibiti wa yasiyotarajiwa ni muhimu katika kutimiza malengo Mungu aliyoweka maishani mwako, ikiwamo kuwa na familia bora, huduma ya kusaidia maisha ya watu, biashara, elimu na kadhalika.

Msomaji wangu, bila shaka maeneo haya mawili ambayo ni kutarajia matokeo makubwa kuliko ulivyowekeza na kutojipanga kwa yasiyotarajiwa, umejifunza hapo kitu fulani kuinua maisha yako. Kadiri unavyowekeza kwa wingi ndivyo utakavyopata vingi. Hiyo ni kanuni!

Vile vile unapaswa kujipanga kwa yasiyotarajiwa kwani kikwazo hicho huna budi kukutana nacho mbele yako. Yapo maeneo ambayo huwa ni vigumu mtu kujua nini kitatokea baadaye, lakini Mungu anajua. Ndiyo maana lipo andiko lake linathibitisha pale anaposema, "kwa kuwa hajui yatakayokuwako; kwa maana ni nani awezaye kumweleza jinsi yatakavyokuwa?"

***Msomaji naishia hapa, sababu zingine wiki ijayo. Kwa maoni tuma ujumbe 0715268581***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Anwani za makazi zilindwe kuepuka kugeuzwa vyuma chakavu

WIZARA ya Habari, Mawasiliano na Tekonolojia ya Habari, kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), inaendelea kuhamasisha uwekaji wa anwani za makazi kwenye mitaa na nyumba mbalimbali nchini.

Kazi hiyo inafanyika kupitia mamlaka za serikali za mitaa ambazo ndizo zina mitaa, vitongoji na nyumba zinazokaliwa na wananchi, lengo ni kurahisisha utambuzi wa watu kwa maana ya nyumba zao na mitaa yao kwa urahisi zaidi.

Kupitia uwapo wa anwani za makazi sasa mtu anaweza kukueleza kwake kwa kukwambia njoo mtaa Fulani, nyumba namba Fulani, hivyo kuondoa utaratibu wa zamani wa kumweleza mtu kuwa nyumba yangu ina rangi fulani au iko karibu na kitu au jengo fulani.

Kwa sasa, hata kwenye Google Map (ramani mtandaoni) mitaa imeingizwa, maana yake mtu anaweza kuandika kwenye anwani yake kuonyesha hadi mtaa anapoishi.

Unapojaza maombi yoyote nje ya nchi utaulizwa namba ya nchi yako yaani +255, jina la mtaa na nyumba namba, mara nyingi Watanzania wengi walishindwa kujaza kwa kuwa havikuwapo lakini sasa vipo na ni wajibu wetu kuzitumia.

Yako maeneo kuna ubishani mkubwa kwamba wananchi hawataki kulipia anwani hizo kwa mfano kibao cha mtaa inatakiwa kuchangiwa Sh. 80,000 na kibao cha nyumba Sh.4, 000. Wanaokataa ni wale ambao hawajaelewa umuhimu wake.

Naamini wakielimishwa wakaelewa namna vina manufaa kwa maisha yao ya kila siku. Wengi wanavichukulia ni vibao tu ambavyo havina kazi yoyote bali serikali inatekeleza mradi wake tu, hivyo ni wa serikali.

Hii inaonyesha elimu inahitajika sana, kwa kuwa wananchi wasiotaka nirahisi hata kuhujumu siyo kwa kuikomoa serikali bali kutoona umuhimu wake.

Kwa muda mrefu Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), inahangaika kushughulikia wanaong'oa alama za barabarani kiasi cha kuamua kuweka vya zege ambavyo bado vimebomolewa na kutoa nondo iliyomo ndani.

Kwingine wamelazimika kuweka chuma kizito ili anayeng'oa au kukata achukue muda mrefu au asiweze kabisa, lengo ni kukabiliana na wahujumu wa miundombinu ya barabara

Licha ya kuwapo sheria ya inayolinda miundombinu, watu bila woga wameendelea kung'oa kwa ajili ya kuuza vyuma chakavu.

Biashara ya vyuma chakavu imeshika kasi nchini hususan mijini ambako watu hupita kutangaza kuwa wananunua vyuma chakavu. Ukiwaita wanakuja na mzani wao wanapima na kununua ulivyonavyo. Wengine wameiba hadi sufuria na vifaa vya watu vyenye chuma na kuviuza.

Sasa kwa anwani za makazi zinazowekwa lazima elimu itolewe kikamilifu,viongozi wa mitaa na vitongoji wahusishwe ili wawe mabalozi wa kulinda, ili inapotokea mtu amehujumu anapopeleka kuuza, mnunuzi akatae kwa manufaa ya nchi yake. Ni muhimu serikali kufuatilia kwa karibu biashara ya chuma chakavu maana tumeona hata miundombinu ya reli na madaraja imehujumuiwa na kwenda kuuzwa kama chuma ambacho huuzwa kwa kilo.

Bila kulinda miundombinu hiyo ambayo ni ya chuma baada ya kumaliza kuweka kutakuwa na kazi ya kukamata wanaong'oa na huenda kuna maeneo vimeshaondolewa.

Nimeona eneo la Kiluvya Hills, vimewekwa vibao vya kimo cha mtoto, vyembamba kiasi cha kujiuliza ndicho kiwango kilichowekwa? Je, kuna kiwango sahihi kilichoandaliwa kwamba anwani zitakuwa zimelingana hivi au vinaruhusiwa kutofautiana?

Kibao kama hicho ni rahisi kuondolewa kwa kuwa hakina uzito,ni bora kuwa na kiwango sahihi,kama ni cha mtaa basi kiwe kama cha alama ya barabarani ambacho ni ngumu mtu kuking'oa na kwenda kukiuza, maana yake itamchukua muda mrefu kung'oa au kukata chuma husika.

Bila kutoa elimu kwa wananchi kupitia kwenye vikao vyao vya mitaa na vijiji ili atakayeharibu akamatwe kirahisi, bila hivyo ikifanyika tathimini baada ya miezi sita mitaa mingi itakuwa haina vibao vilivyowekwa kwa gharama kubwa. Lazima wananchi wajue ndiyo utaratibu wa kidunia, nimeshatembelea Marekani, Ulaya na Asia kote mitaa ina vibao vizuri vya kisasa vinavyoonyesha mitaa husika jambo linalompa mgeni urahisi kujua anakoenda.

Ndiyo maana leo hii unaweza kwenda mji fulani ukapewa ramani ikakusaidia, au ndiyo maana wanapokuja wageni kutoka nje hupenda kutumia ramani kwenda maeneo na sasa ulimwengu wa kidigitali umeleta Google map (ramani mtandaoni) itakayomwelekeza mtu kufika anapotaka kwenda.

***Mungu ibariki nchi yangu.***

> **"Hii inaonyesha elimu inahitajika sana, kwa kuwa wananchi wasiotaka nirahisi hata kuhujumu siyo kwa kuikomoa serikali bali kutoona umuhimu wake.**

# HARUSI





Pambo la maua limekuwa maarufu katika harusi mbalimbali duniani, hata hivyo kuna aina nyingi ya ubebaji wa maua katika sherehe kama inavyoonekana katika picha.







# MITINDO







# Mavazi ya mazoezi

MAZOEZI ya mwili yanazidi kuzingatiwa katika makundi ya watu, kiasi kwamba umekuwa kama utaratibu wa kila siku.

Sababu za mazoea ya watu kufanya mazoezi ni tofauti kama urekebishaji wa mwili kimatibabu, urembo na michezo.

Lakini kuna swali: Je! Nguo za mazoezi sahihi ni bora kuliko nguo za kawaida? Je! Nguo zinazofaa kwa mazoezi ya mwili zinaweza kuwa na faida yoyote ?

Majibu ya maswali yote ni ndio, kwani nguo za mazoezi zilizo sahihi zina faida kubwa katika ufanyaji wa mazoezi.

**Blauzi, fulana na jaketi**

Wanaochukua mazoezi ya kujenga mwili ni lazima kutumia nguo zinazoruhusu mzunguko mzuri wa jasho. Kumbuka kwamba mwili unavyozidi joto, ndivyo unavyopoteza maji na zaidi mlo bora kwa kupoteza-uzito kuruhusiwa vyakula-na-virutubisho utendaji huanguka.

Unatakiwa kuvaa fulana za mikono mirefu, blauzi au jaketi isiyobana mwili. Mavazi haya yanatakiwa kuwa mepesi, hazipaswi kukufanya uwe na wasiwasi juu ya chochote.

**Viatu**

Viatu vikubwa na vizito vinaweza kukupa tabu wakati wa mazoezi, unatakiwa kuvaa raba nyepesi zenye uwezo wa kukufanya uwe mwepesi kufanya chochote ndani ya ukumbi wa mazoezi.

UREMBO



# Kabiliana na mionzi ya jua

MAISHA yetu ya kila siku ya kutafuta riziki na mambo mengine, hatuwezi kukwepa mionzi ya jua.

Mionzi ya jua sio tu huzifikia ngozi zetu, lakini pia huweza kusababisha mabadiliko katika ngozi na kusababisha kufifia au kuwa nyeusi zaidi.



Pia husababisha mtu kuwa na rangi zaidi ya moja kwenye mwili wake, kuanzia ya usoni kutofautiana na ya ndani ya mwili wake.

Suluhisho la tatizo hili sio kupaka vipodozi vyenye kemikali, bali kutumia njia zifuatazo za asili ili kusaidia kuondoa utofauti wa rangi.

**Nyanya na Asali**

Mahitaji ni nyanya kubwa moja na asali kijiko kikubwa.

Kuna njia mbili unazoweza kutumia kuandaa, moja chukua nyanya, ikate katikati na uchovye asali upande huo ulioukata kisha anza kupaka sehemu husika.

Lakini ya pili, chukua nyanya uisage na kisha changanya asali na uanze kupaka. Subiri kwa dakika 15 hadi 20 baada ya hapo nawa maji halafu jikaushe kwa kitambaa safi.

Fanya hivi kila siku kupata matokeo yanayo ridhisha.

**Tango na Asali**

Mahitaji ni tango moja, asali kijiko kimoja cha chai.

Saga tango kisha changanya na asali. Paka mchanganyiko huu sehemu iliyoathiriwa, subiri kwa dakika 10 hadi 15 kisha nawa maji. Tumia njia hii mara moja au mbili kila siku.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Utamu wa vitumbua vya nyama



WATU wengi wamezoea kupika au kula vitumbua vya mchele, leo katika safu yetu ya mapishi tutaelekezana namna ya kupika vitumbua vya nyama.

Vitumbua hivi havipikwi kwa kutumia unga wa mchele kama tulivyozoea vitumbua vingine isipokuwa nyama ya kusaga.

Ni pishi zuri sana, ukiwa na juisi pembeni, vinapendeza kula muda wa jioni, ila waweza kula muda wowote wa nafasi yako.

**Mahitaji**

Nyama ya kusaga robo, kitunguu kimoja, kitunguu saumu nusu kijiko, karoti moja, pilipili hoho nusu, mayai matano hadi sita, baking powder nusu kijiko kidogo, pilipili manga kiasi, pilipili mbichi na chumvi kiasi

**Namna ya kupika vitumbua**

Safisha nyama, uiweke saumu, chumvi, pilipili manga na tangawizi, ibandike jikoni ili iive na ikauke vizuri.

Kata vitunguu, hoho, pilipili na uvichanganye na mayai, kisha vyote vitie kwenye nyama yetu.



Weka kwenye blender mchanyanyiko wetu uusage kidogo ila usiwe laini sana. Ikiwa tayari, mimina katika bakuli.

Kisha tia baking powder, karoti na chumvi kidogo kisha changanya vizuri.

Andaa chuma cha kukaangia vitumbua, bandika jikoni, weka mafuta kidogo.

Mafuta yakipata joto chota kwa upawa mchanganyiko wetu utie kwenye kikaango, vikiiva upande mmoja geuza na upande wa pili uive kisha uvitoe.

Endelea kuchoma hadi viishe vyote, hapo tunakua tumemaliza upishi wetu wa vitumbua

Vitumbua vyako vitakuwa tayari kwa kuliwa wakati wowote utakaojisikia kwa juisi, soda au kinywaji ukipendacho.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



## Namna ya kutumia Rice Cooker kuokea mkate




KILA kitu unachotumia jikoni mwako kinaweza kufanya kazi zaidi ya moja inategemea na ubunifu wako na kitu husika.

Hii inaweza kudhihirika zaidi pale unapoweza kuandaa vyakula vya aina mbalimbali kwa kutumia chombo aina ya 'rice cooker' ambacho wengi wanatumia kupikia wali.

Hata hivyo kwa kutumia 'rice cooker' unaweza kuoka keki au mkate, badala ya kutumia oven.

Kabla ya kuoka hakikisha unaziba tundu la kutolea mvuke, hii itafanya joto lisipotee na kuifanya keki iive vizuri zaidi.

**1.** Fuata maelekezo yote kama yalivyo kwenye kuandaa unachotaka kuoka.

**2.** Weka mchanganyiko wako kwenye rice cooker. Fanya kama unavyopika wali na kisha washa jiko liwe kwenye "On Mode".

**3.** Ili kupata matokeo bora, hakikisha hupotezi joto litakalokuwa kwenye rice cooker, hivyo funika na mfuniko usio na tundu, au ziba tundu la mfuniko.

**4.** Kama ilivyoelezwa, joto la rice cooker halifanani na lile la oven. Hivyo basi, inatakiwa muda mrefu kiasi tofauti na oven, muda unaokubalika si chini ya saa moja.

# Kumbe nyumba nazo hukumbwa na fangasi!

KAMA ilivyo changamoto katika kila jambo kwenye maisha ya binadamu na katika kila tunachokifanya, kadhalika na kwenye sekta ya nyumba ni vivyo hivyo.

Miongoni mwa mambo yanayosababisha changamoto katika eneo hilo ni pamoja na kutokufanya uchaguzi sahihi wa uwanja wakati wa kununua kwa ajili ya ujenzi wa nyumba husika, kwa kukosa ushauri au kwa sababu nyinginezo.

Fangasi kwenye nyumba ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazoharibu nyumba nyingi.

Mtaalamu wa masuala ya ujenzi, Joseph Nyamihonga, anasema chanzo cha fangasi kwenye nyumba ni hali inayosababisha majengo kuoza kutokana na kuathirika na hali ya unyevunyevu wenye kemikali mbalimbali zilizopo kwenye ardhi.



Anasema fangasi husababishwa na kuwapo kwa hali ya majimaji kwenye nyumba kwa muda mrefu kutokana na uwapo wa chemchem, mvua au matumizi ya maji mengi katika eneo la nyumba.

Nyamihonga anasema tatizo hilo husababisha kuoza kwa kuta, sakafu, nondo na malighafi mbalimbali kwenye nyumba pamoja na kuchochea nyumba kushambuliwa na mchwa baada ya kuozeshwa na unyevunyevu uliopo.

Anataja baadhi ya sababu kuu za majengo kupata fangasi kuwa ni pamoja na kutozingatia vigezo vya usanifu wa nyumba.


"Katika safari yangu ya kitaaluma nimefundishwa kuwa ujenzi unaweza kufanyika mahali popote kwenye ardhi maadamu umezingatia vigezo vyote kukidhi hali ya mazingira ya eneo la ujenzi, ujenzi holela unaoendelea kufanyika unasababisha hasara na hali ya wasiwasi kubwa katika ubora na usalama wa wakazi.

"Wengi wetu tumejenga maeneo yenye ardhi ambayo muda wote wa majira huwa imetota maji ambayo huwa yana mchanganyiko wa kemikali mbalimbali za kimazingira na nasikitika kusema wengi hawakufuata taratibu za kisanifu hali inayosababisha kuoza kwa majengo na hatimaye kuchakaa haraka," anasema.

Kwa mujibu wa Nyamihonga, sababu nyingine inayochangia tatizo hilo ni kutumia malighafi zisizo na ubora, kutozingatia utaalam wakati wa ujenzi.

Anasema usanifu wa majengo huratibu mfumo na muundo wa nyumba ili iweze kupambana na mazingira husika, ikiwamo hali ya majimaji ili kuzuia isikaribishe madhara yoyote kwenye nyumba.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... ...BEI ITAPANDA KILA SEHEMU LAKINI HAIWEZI KUPANDA MLIMA...

# Mbunge Kenya ashtakiwa kughushi vyeti

**NAIROBI,** KENYA

MBUNGE wa Kenya anatuhumiwa kughushi vyeti vya sekondari baada ya kubainika hakufanya mitihani yake ya mwisho katika shule ya upili anayodai kuwa alisoma

Mbunge huyo, Oscar Sudi, alisema kwamba alifanya mitihani hiyo katika Shule ya Sekondari ya Highway mwaka wa 2006. Lakini mkuu wa zamani wa shule hiyo, alipinga kauli hiyo akieleza namba ya mtihani ambayo Sudi alisema ilikuwa yake ni ya mwanafunzi mwingine.

Aliongeza kwamba mbunge huyo hakujisajili wala kufanya mtihani shuleni hapo.

Mbunge huyo ameshtakiwa kwa kughushi cheti cha stashahada na cheti cha shule ya upili. Lakini mwenyewe amekataa mashtaka na yuko nje kwa dhamana.

Kulingana na gazeti la Standard la Kenya, madai hayo ya kughushi yalianza tangu alipokuwa akitafuta kibali cha uchaguzi mwaka wa 2013, ambapo sheria iliwataka wagombea ubunge kuonyesha uthibitisho wa elimu ya baada ya sekondari.

# Mwili wakutwa katika njia ya ndege

**LOGOS,** NIGERIA

MAMLAKA ya Uwanja wa Ndege wa Nigeria, inachunguza baada ya mwili wa binadamu kukutwa kwenye barabara ya kurukia ndege katika uwanja mkuu wa ndege jijini Lagos.

Mtu huyo ambaye hajatambuliwa aligunduliwa wakati wa ukaguzi siku ya Alhamisi majira ya asubuhi.

Mamlaka hiyo ilisema njia ya kurukia ndege ilifungwa kwa takriban saa mbili na nusu ili kuruhusu maiti kuondolewa.



Baadhi ya Wanajeshi 531 wa mwisho wa Ukraine wakiwa katika basi maalum wakiondolewa katika mji wa Mariupol baada ya vikosi vya Russia, kufanikiwa kuwatoa ndani ya kiwanda cha chuma walimojificha kwa miezi minne. **PICHA: REUTERS**

# Russia yatangaza kushinda vita na kuudhibiti mji wa Mariupol

## ■ Wanajeshi 531wa mwisho wajisalimisha

**MARIUPOL,** UKRAINE

HATIMAYE Russia waumeudhibiti mji wa Mariupol baada ya wapiganaji 531 wa mwisho wa Ukraine, waliojificha katika eneo la kiwanda cha chuma cha Azovstal, kujisalimisha.

Kwa miezi kadhaa vikosi hivyo vilikuwa vimezingirwa katika jengo hilo kubwa, na kuzuia wanajeshi wa Russia kushindwa kuudhibiti kamili mji huo.

Uokoaji uliofanyika juzi unaashiria mwisho wa kuzingirwa na uharibifu zaidi katika mji wa Mariupol ambao sasa umesalia magofu.

"Vituo vya chini ya ardhi vya kiwanda hicho, ambako wanamgambo walikuwa wamejificha, viko chini ya udhibiti kamili wa majeshi ya Russia," ilisema taarifa ya Wizara ya Ulinzi.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alisema walinzi wa mwisho waliosalia katika eneo hilo wameruhusiwa kuondoka.

"Leo wapiganaji hao walipokea ishara ya wazi ya amri ya kijeshi kwamba wanaweza kutoka nje na kuokoa maisha yao," alikiambia kituo cha televisheni cha Ukraine mapema juzi.

Kwa wiki kadhaa eneo hilo la Azovstal lilikuwa limezingirwa kabisa, huku vikosi vya Russia vikihakikisha hakuna kitu kinachotoka au kuingia ndani ya kiwanda hicho.

Aidha, vilizuia misaada yote ya kibinadamu kuingia, na kulishambulia eneo hilo kutoka angani na kuwataka watetezi wake waliobaki kuweka chini silaha zao na kujisalimisha.

Wengi wa wale waliokwama ndani walikuwa raia, ikiwa ni pamoja na wanawake, watoto na wazee.

Baadhi waliondolewa mapema mwezi huu, kufuatia mazungumzo magumu yaliyoratibiwa na Umoja wa Mataifa na Shirika la Msalaba Mwekundu ambayo yalidumu kwa wiki kadhaa.

Lakini kuendelea kukataa kujisalimisha kwa wapiganaji hao wa Ukraine kulimaanisha Russia haikuweza kuwa na udhibiti kamili wa mji huo wa bandari ya kimkakati.

Kwa raia wengi wa Ukraine, inawaona wapiganaji hao wa Azovstal waliojisalimisha kama mashujaa wa kitaifa ambao walionyesha upinzani dhidi ya Russia.

Mamia ya wanajeshi waliojificha kwenye mahandaki ya kiwanda hicho ni pamoja na wanamaji, Jeshi la Ulinzi la Taifa ikiwa ni pamoja na kikosi cha Azov, walinzi wa mipaka, polisi na vitengo vya ulinzi wa eneo hilo.

Walipiga kambi ndani ya kiwanda hicho wakiishi kwa shida bila chakula cha kutosha na maji kwa wiki kadhaa chini ya ardhi kwenye mahandaki bila kuona mwanga wa jua.

**RUSSIA YASITISHA GESI KWA FINLAND**

Russia imesitisha usambazaji wake wa gesi asilia kwa Finland, kampuni ya nishati inayomilikiwa na serikali, Gasum ilisema katika taarifa yake.

Sababu ya kufungwa kwa bomba la gesi inatokana na Finland kukataa kununua nishati hiyo kwa sarafu ya ruble na kufuatia kuomba uanachama wa Nato.

Kampuni ya Gasum ilisema hatua hiyo ni ya kusikitisha, lakini haitakuwa na usumbufu kwa wateja.

Licha ya mzozo wa Ukraine, Russia inaendelea kusambaza gesi katika nchi nyingi za Ulaya.

Baada ya mataifa ya Magharibi kuiwekea vikwazo Russia, kutokana na vita hivyo, ilizitaka nchi zisizo rafiki lazima zilipe gesi kwa kutumia sarafu ya Russia, hatua ambayo Umoja wa ulaya ilichukulia kama kulazimisha kwa kutoa vitisho.

Kutegemea nishati ya Russia ni sababu inayochangia katika kupanda kwa gharama za maisha kunakowakabili watumiaji wengi.

Finland inaagiza gesi yake nyingi kutoka Russia, lakini gesi inachukua chini ya kumi ya matumizi ya nishati nchini humo.

"Inasikitisha sana kwamba usambazaji wa gesi asilia chini ya mkataba wetu wa usambazaji sasa utasitishwa," Mkurugenzi Mtendaji wa Gasum Mika Wiljanen alisema.

Aliongeza "Hata hivyo, tumekuwa tukijiandaa kwa umakini kukabiliana na hali hii na kwa kuzingatia kwamba hakutakuwa na usumbufu katika mtandao wa kusambaza gesi, tutaweza kuwapa wateja wetu wote gesi katika miezi ijayo,"

Alipoulizwa kuhusu suala hilo, msemaji wa Kremlin alisema "Ni dhahiri kwamba hakuna mtu atakayepewa chochote bure".

Awali, Russia ilikata usambazaji wa umeme kwa Finland. Ikiitishia kulipa kisasi iwapo nchi hiyo itajiunga na Nato.

**BBC**

## MAKALA

# HUDUMA KATIKA OFISI ZA UMMA



Na Magabilo Masambu - 0689157789

KUNA tofauti kubwa kati ya binadamu na mtu. Kila mtu ni binadamu lakini si kila binadamu ni mtu. Sababu kubwa ni kwamba ukiwa binadamu ukakosa utu u tabakia kuwa binadamu tu. Lakini binadamu mwenye utu ataitwa mtu kwa sababu ya utu wake. Utu huonyeshwa kwa namna mbalimbali kama vile kauli nzuri kwa wengine, huruma, kujali, kuona matatizo ya wengine kama yako.

Niliwahi kusoma mahala fulani hadithi ya mtu mmoja anaitwa Msamaria. Kuna mtu mmoja alikuwa anasafiri kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko, akiwa njiani akavamiwa na majambazi wakamchania nguo na kumpiga kisha wakamtupa barabarani akiwa katika hali ya kufa. Siku hiyo ilikuwa ya ibada, hivyo watu wengi walikuwa wakipita katika ile njia kwenda katika nyumba ya ibada, miongoni mwao walikuwamo pia viongozi wa dini.

Yule aliyeumizwa alikuwa amelazwa katikati ya barabara, hivyo kila aliyefika hapo alipita pembeni yake ikiwa hivyo hata kwa wale viongozi wa dini, huku wakionekana kuwahi ibadani.

Lakini baadaye bwana mmoja, alipofika eneo lile akasimama akamtazama, akamhurumia. Akagundua kuwa aliumia vibaya na alihitaji msaada wa matibabu. Akamsafisha majeraha kwa mafuta ya Mzeituni na divai kisha akamchukua akampandisha juu ya punda wake na kumpeleka mpaka nyumba ya wageni, akamhudumia huko.

Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, huwezi kuwa na kauli au lugha nzuri kwa wale unaowahudumia kama ndani mwako hakuna roho ya utu. Huwezi kumkuta mtu ameumizwa au anahitaji masaada wako ukamsaidia kama vile vile huna roho ya utu ndani mwako. Utu unaweza kuwa tabia ya kuzaliwa ama kujifunza au inaweza kuwa imetokana na malezi. Kama ambavyo watu hujifunza ubaya, vilevile uzuri na utu hufunzwa. Kisa cha msamaria kinaweza kutufundisha jambo kuhusu kuwahudumia wahitaji.

Maeneo mengi ya kazi, tabia mbalimbali za watu huthibitiwa kwa kutumia sheria. Hii ni kusema kwamba sheria zipo kwa ajili ya wakaidi na wasiopenda kufuata utaratibu. Kuna mambo pamoja na kuthibitiwa na sheria, bado ni vigumu kuhakikisha kila mmoja anafuata taratibu ikiwa ni pamoja na kujali, kuheshimu na kuwakirimu watu ofisini kwa sababu mambo mengine yanatokana na tabia za kuzaliwa kama ambavyo waswahili wasemavyo kwamba tabia ni kama ngozi kubadilika huwa ni kazi kubwa.

Katika mambo yanayotajwa kama mafanikio makubwa ya serikali ya awamu ya tano chini ya utawala wa Hayati John Pombe Magufuli, mojawapo ilikuwa kujenga nidhamu ya watumishi wa umma katika kuwahudumia wananchi. Sasa hoja pengine inaweza kuwa kwamba watu walikuwa na nidhamu ya woga, sawa, lakini kama hiyo nidhamu ya ilifanya kazi, basi haina budi kujengwa kwa sababu tunachotamani kuona ni watumishi wa umma wakiwatendea mema wananchi.

Kwa kuyasema haya, sina maana kwamba kwa sasa hakuna nidhamu hiyo. Wako watumishi waaminifu kabisa ambao wanafanya kazi vizuri na wanastahili pongezi ili waendelee kufanya vizuri zaidi. Lazima tukubali kwamba kukuwapo na baadhi ya maeneo, baadhi ya viongozi na watumishi wameanza kujiona kama miungu watu, tunataka kurudishwa katika enzi zile za kuabudu watu kwanza ndipo watuhudumie.

Kuna kila sababu za hatua stahiki kuchukuliwa ili kulinda heshima ya serikali kwa wananchi. Kuna wakati tulikuwa tukihudumiwa mpaka tunaulizwa kama tumeridhika na huduma. Sina hakika kama leo hii tunaulizwa tena. Kama wako watumishi wa aina hiyo, basi Mwenyezi Mungu awabariki sana. Ninasema bado wako hao wachache kwa sababu ninao ushuhuda wa dada mmoja ambaye ni mlinzi katika ofisi za jiji la Arusha.

Dada yule anapaswa kuwa mfano wa kuigwa na kama tungalikuwa tukihudumia watu kwa namna ile, basi wengine wangalikuwa wanapona kabla ya kumwona daktari.

Hiyo ni hulka ya mtu kwa nini wengine tunashindwa kuwa hivyo? Tunapoteza nini tunapokuwa na kauli nzuri kwa wateja wetu. Kwa nini tusubiri vitisho au adhabu ndiyo tuwahudumie watu vizuri?

Fikra tuliyo nayo vichwani wengi wetu ni kudhani kwamba sisi ndio tumekuwa watu wa kwanza na tutakuwa wa mwisho katika ofisi zetu tulimoajiriwa.

Unapopata nafasi ya kutumika hasa katika ofisi ya umma, tambua kwamba wako wengi wamepita hapo na hawajawahi kudumu ndiyo maana wewe umepata nafasi hiyo. Kiburi, dharau, majivuno na kauli za ovyo kwa wale unaowahudumia mwisho wa siku zitakufikisha pabaya.

Natambua kwamba ni kweli sisi kama binadamu tuna mapito mbalimbali. Unaweza kuwa umekwazwa, unadaiwa mikopo, una matatizo ya kifamilia chungu nzima lakini jambo muhimu kufahamu ni kwamba hayo matatizo uliyo nayo hata wengine wanayo tena pengine makubwa zaidi kuliko yako. Hata hivyo, yote wanayaacha nje ya ofisi na ukiwakuta wanahudumia watu huwezi kujua kama wana matatizo. Hii ni kwa sababu wale unaowahudumia si sehemu ya matatizo yako. Huna sababu ya kuwakasirikia bali unapaswa kupambana na hali yako nje ya ofisi ya umma.

Ni kweli kwamba katika kutoa huduma hutamridhisha kila mtu, lakini utakuwa mtu wa ajabu sana kila mtu kukusema kwa mabaya juu ya huduma zako.

Wako wanaopenda kuonekana wakali ikiwa ni sehemu ya kujikinga ili wasifahamike udhaifu walio nao kwenye utendaji, hivyo kazi yao ni kutisha watu mpaka watumishi wenzao ili asihojiwe au kuulizwa mambo fulani na watu wa sampuli hizi huwa ni wezi, wabadhirifu na kadhalika. Maisha haya ni mafupi sana kuliko tunavyodhani, furaha huongeza maisha lakini pia ufanisi wa kazi unakuwa wa hali ya juu.

Ukishaanza kugombana na unaowahudumia kwa vyovyote utaharibu kazi zako za kila siku.

Ushauri wangu, tumsaidie Rais na serikali yake ili asionekane ameshindwa kuwasimamia watumishi. Kila mtu ana hulka yake katika uongozi yeye hawezi kuwa kama yule.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Ashibaye', wimbo wa kwanza wa TX Moshi Msondo Ngoma



Na Adam Fungamwango

LEO nitamzungumzia mwanamuziki aliyeibukia kuwa nyota nchini Tanzania mwishoni mwa miaka ya 1970 hadi alipofariki dunia Machi 29, 2006 kwenye Hospitali ya Muhimbili, Dar es Salaam.

Huyu si mwingine bali ni Moshi William, ambaye baadaye alipachikwa jina la TX na mtangazaji mahiri wa Radio Tanzania Dar es Salaam wakati huo, Julius Nyaisanga.

Nyaisanga alimpachika jina hilo ambalo liling'ang'ania na kuonekana kama vile amezaliwa nalo kiasi kwamba huwezi kutaja jina lake bila kuanza na TX kutokana na kumchukulia kama ni mtaalam kutoka Polisi Jazz Band, aliyekuja kuibeba JUWATA Jazz Band, wana Msondo Ngoma.

Zamani kwenye miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990, wataalam kutoka nje ya nchi, magari yao wanayotembelea yalikuwa na namba zao maalum, yanayoanzia na TX. Ni kama vile magari ya serikali yanavyoanzia na ST, binafsi T, Jeshi la Polisi P na Jeshi la Wananchi JW.

Kirefu chake ilikuwa ni Tanzania Expert na miaka ambayo Moshi anajiunga na Msondo ndiyo namba hizo zilipoanza kuwekwa kwenye magari ya wataalam hao. Ndipo Nyaisanga alipompachika jina hilo akiwa na maana kuwa ni mtaalam aliyetoka Polisi kwenda Msondo.

Na hii ni baada ya Shaaban Dede kuondoka Msondo na kwenda kujiunga na Mlimani Park Orchestra, ndipo Moshi alipoletwa Msondo mwaka 1982.

Kilichotokea ni kama utani tu, Moshi ambaye alikuwa tayari askari wa Jeshi la Polisi lakini ilionekana kwake muziki ulikuwa kwenye damu, kuliko uaskari wake. Wengi hawajui kuwa kama asingejiunga na Msondo, basi angeweza kuwa mwanamuziki wa bendi ya Vijana Jazz. Na Tx Moshi alishawahi kupigia kwa muda bendi ya UDA Jazz.

Mwanamuziki huyo aliyezaliwa Hale, mkoani Tanga mwaka 1958, alikwenda kutafuta maisha jijini Dar es Salaam katikati ya miaka ya 1970 na kukutana na Benovilla Antony ambaye alikuwa amekabidhiwa mikoba ya kuanzisha bendi ya UDA Jazz.

Hata hivyo, wanamuziki wa bendi hiyo ni lazima wawe wafanyakazi, hiyo ilimfanya Moshi na wanamuziki wenzake, kuanza kazi ya kufyeka majani eneo ambalo lilikuja kuwa ni maegesho ya mabasi aina ya Ikarus yanayofanana sana kwa sasa na mabasi ya mwendokasi yenye trela. Baadaye ndilo eneo ambalo lilikuwa ni stendi ya mabasi kwenda mikoani eneo la Ubungo, Dar es Salaam.

Hakukaa sana na bendi hiyo, akaamua kurejea Tanga. Alirejea tena Dar es Salaam, baada ya kutokea tafrani na vijana wenzake Hale. Aliamua kutoroka na alipofika, alijiunga na Polisi Jazz Band kwa msaada wa mwanamuziki mwenzake mmoja aliyekuwa naye UDA Jazz, ambaye aliwaambia wenzake kuwa ni mwimbaji mzuri sana.

Nyimbo kama 'Wivu Sina', 'Mayasa', 'Dunia' na 'Mwaka wa Wato', zilimpatia umaarufu mkubwa kiasi cha bendi mbalimbali kubwa kuanza kumuwinda. Aliathiriwa na uimbaji wa George Peter Kinyonga wa Simba Wanyika, ambaye yeye na kaka yake, Wilson Peter, waliishi wote eneo ambalo Moshi pia aliishi Hale, Muheza mkoani Tanga, wakicheza na kukua wote, ingawa kina Kinyonga walikuwa wakubwa kidogo kuliko yeye.

Mwenyewe alikiri wakati wa uhai wake kuwa anaimba kwa kumuiga George, mwanamuziki ambaye anampenda sana na ndiye alikuwa kioo chake kwenye muziki.

Wakati wa tamasha moja la Kichama viwanja wa Mnazi Mmoja mwishoni mwa miaka ya 1970, bendi nyingi zilikutana zikiwapo zile kubwa. Polisi Jazz walipiga wimbo kopi wa Simba Wanyika uitwao 'Baba na Mama', Moshi aliimba kwa ustadi mkubwa na kushangiliwa mno na mashabiki kiasi cha kuwashangaza hata kina Marijani Rajabu na Hemed Maneti ambao walikuwa na bendi zao.

Hapo ndipo Maneti alipomnyemelea na kumpata, akampeleka Vijana Jazz Band. Hata hivyo askari Polisi walivamia mazoezi ya bendi hiyo kumsaka mwanamuziki wao, na aliwekwa rumande kwa kosa hilo, huku bendi ya Vijana ikionywa. Mashabiki wa Polisi Jazz nao hawakukubali kufanya onyesho bila kuwepo Moshi. Akasamehewa na kupelekwa jukwaani ili kuepusha fujo za mashabiki.

Juwata Jazz Band ilifanikiwa kumng'oa Moshi Polisi baada ya yeye mwenyewe kufuata taratibu zote, ilikuwa ni pamoja na kuandika barua ya kuacha kazi. Alipofika Msondo mwaka 1982, alikuta wimbo ambao ulikuwa umeshafanyiwa mazoezi na kuimbwa na Dede kabla ya kutimkia Sikinde. Ulikuwa utunzi wake Kassim Mponda unaitwa 'Ashibaye'. Ilibidi auimbe yeye, na ndiyo wimbo wa kwanza kabisa kwa Tx Moshi kuuimba alipoingia kwenye bendi hiyo.

Wimbo wa kwanza kutunga Msondo ni 'Hamida', ambao alimtungia mkewe, Asha Mwanasefu, ambaye pia hilo ni jina lake, hata wimbo wa 'Cheusi Magala' pia aliimuimba mkewe huyo huyo na Magala ni jina la nyumbani kwao Unyamwezini.

Kwa miaka mitatu mfululizo, 2003, 2004, na 2005, TX Moshi alitunukiwa tuzo ya kitaifa ya utunzi bora. Tangu ajiunge na Msondo, ndiye mwanamuziki waliyetunga zaidi ya robo tatu ya nyimbo zote za bendi hiyo.

Kifo chake kilitokana na majeraha ya mguu aliyoyapata kutokana na ajali ya gari maeneo ya Mivinjeni karibu na nyumbani kwake Keko Machungwa.

Pamoja na kwamba hayakumfanya kuacha kuendelea na kazi ya muziki hadi kutoa albamu ya 'Ajali', yenye wimbo unaozungumzia tukio hilo. Lakini miezi kadhaa baadaye alizidiwa na kufariki dunia. Akiacha vilio, majonzi kwa mashabiki wa muziki wa dansi, si wa Msondo tu, bali Afrika Mashariki nzima.

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na wanapomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofikia umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-2

**Na Adam Fungamwango
(0716 350534)**

MWANANGU kwenye dunia hii, adui yako ni yule unayekula naye. Hakuna mtu yeyote anayeweza kukudhuru ambaye hakujui. Ataanzia wapi? Asiyekujua hawezi kuwa karibu na wewe. Ili mtu akudhuru, jambo la kwanza ni lazima awe karibu na wewe.

Ndiyo maana siku zote nakwambia, usiwe sana na ukaribu na watu. Mtu anaanza kwanza kuwa karibu na wewe, halafu ukishamuamini, ndipo anatumia fursa hiyo kukudhuru.

Wale waliosema kikulacho ki nguoni mwako hawajakosea. Kunguni wanaokung'ata wako kitandani mwako, hawawezi kufanya hivyo kama wapo kwenye kitanda cha mtu mwingine." Pokwa aliendelea na tabia yake ya kumjaza falsafa zake kijana wake Prince. Naye alikuwa ameshashiba, kuzizoea na kuziishi.

"Maisha yote unayoishi, ingawa unaishi kwenye nyumba nzuri, unapata kila kitu, baba yako nina mali nyingi, lakini upweke huu tulionao mimi na wewe, unasababishwa na watu kama hawa.

Unasababishwa na mzee Sabri na wenzake. Mwanangu nenda kwanza kammalize. Ukifanikiwa nitajua sasa umekua. Umekua mkubwa, na hapo nitakueleza kila kitu."

Maneno yaliingia kwenye ubongo wa Prince. Hana hajui ndugu yeyote wa mama yake, hamjui mama yake. Hana kaka, dada wala ndugu wa damu. Kumbe ni kwa sababu ya Sabri? Damu ilianza kumchemka mwilini.

Damu ilianza kumchemka mwilini. Akapeleka mkono mezani na kuinua bastola yake. Akaitazama. Akaibusu.

"Nitakwenda baba, nina hamu sasa ya kutaka kujua juu ya familia yangu.

Mama yangu, ndugu zangu na kila kitu kilichojificha ambacho unataka kuniambia."




**Tangu mdogo ilikuwa ndiyo kazi yake. Anakumbuka kila Jumamosi na Jumapili, kazi ilikuwa ndiyo hiyo. Awali ilikuwa ngumu, lakini kadri muda ulivyozidi alianza si tu kuizoea, bali kuipenda pia. Kwake ilianza kuwa kama mchezo wa kitoto.**

********************************

Saa tatu usiku, tayari Prince alikuwa ameshatia timu. Eneo la Ilala Bungoni lilionekana kawaida tu kama siku zote. Hakuna aliyemtilia mashaka kijana mmoja aliyevaa jinzi la bluu lililochakaa na kupauka, kiasi cha kupoteza uhalisia wa rangi yake na kuonekana kana jeupe. Lilikuwa limechanwachanwa magotini, akiwa amevaa raba.

Prince alimsifu baba yake mzee Pokwa kwani jinsi alivyomueleza na ramani aliyoikuta ilikuwa ni vile vile.

Alishaliona duka kipindi kirefu, lakini alikuwa akizungukazunguka kupoteza muda. Alikuwa akielekea upande mmoja na kurudi, kama vile mtu aliyepotea sehemu.

Alifika sehemu moja inayouzwa pweza, alisimama na kuanza kula kama wengine aliowakuta. Ilipotimu saa nne kasorobo alikuwa mita chache tu kutoka kwenye windo lake.

Mlengwa alishamuona kitambo. Alikuwa mzee mmoja mwenye asili ya karabu. Alishaambiwa kuwa jina lake ni mzee Sabri.

Gari alilokuja nalo Toyota IST akuwa ameliweka mbali sana, karibuni kabisa na Amana Social Club. Lengo ni kwamba akimaliza kazi yake asiwe mtu wa kuingia ndani ya gari na kuondoka, kwani anaweza kushtukiwa.

Kwa mbali aliona gari jeupe aina ya Toyota Yaris ikitembea ikija taratibu eneo ambalo yupo na kusimama nje ya duka la mzee Sabri.

Nywele zilianza kumsisimka. Alijua tayari muda wa kazi umewadia. Alivuka ng'ambo ya pili ya barabara na kukaa mkabala na duka hilo ili aone vizuri. Amuone vizuri mzee Sabri atakavyokuwa akitoka nje.

Sekunde chache baadaye akajiona hakukaa sehemu sahihi. Ni sehemu ambayo mzee Sabri anaweza kutoka dukani na kuingia ndani ya gari bila yeye kumuona. Ni kwa sababu upande alisimama ndipo yupo dereva.

Ilibidi avuke tena barabara ili amuone vizuri mzee Sabri atavyokuwa akitoka dukani.

Akachagua sehemu nzuri tu. Aliyekuwa akiendesha gari alitoka. Alikuwa ni kijana ambaye umri haukupishana na yeye, ila mwenzake alikuwa na asili ya kiarabu.

Mzee Sabri naye akatoka. Kilichoonekana ni kwamba walikuwa wanasaidiana kufunga duka. Ni aina ya mageti ambayo ni maarufu kwenye maduka ya biashara, yanayofunguliwa chini kwenda juu na wakati wa kufunga, unavuta kutoka juu kuja chini.

Wakati mwingine unatakiwa utumie nguvu kubwa kama reli za geti lenyewe hazina grisi ya kutosha.

Sabri wala hakujiuliza kugundua kuwa atakuwa mmoja kati ya kijana wake, kwani tayari alishaambiwa na baba yake kuwa huja kuchukuliwa usiku na watoto wake.

Alijipapasa kwenye mfuko wa nyuma kuhakikisha kama bastola yake ipo. Kama alivyotarajia. Aliichomoa taratibu akiangalia huku na huko kuona kama kuna mtu anamtazama. Haikuwa hivyo. Kila mtu alikuwa na mambo yake. Usiku nao ulisaidia. Hata aliyepita karibu hakuweza kuhisi kama iliyokamatwa mkononi ni bastola.

Wakati dereva kijana akifungua mlango kuingia ndani ya gari, baba yake ambaye alikuwa amechelewa kidogo. Alikuwa ni kama anatuma meseji hivi. Kujichelewesha huko kulimfanya Prince atabasamu. Ndicho alichohitaji. Mlango wa dereva ulifungwa, sasa aliyebaki ni Sabri.

Mkono wake ulipokuwa unafungua mlango, ndiyo sekunde hiyo hiyo, alipobonyeza kitufe cha bastola.

Risasi ilikwenda moja kwa moja kwenye kichwa cha mzee Sabri na kumrusha hatua kadhaa mbele. Mlio mkubwa wa bastola ulisababisha watu mbalimbali waliokuwa maeneo jirani waanze kukimbia ovyo bila ya kujua wanapokimbilia.

Hiyo ilimpa fursa nzuri, Prince kujichanganya, akijifanya na yeye ni mmoja kati ya watu waliohamanika na kusikia sauti kali ya mlio huo wa ghafla.

Moja kwa moja alikwenda hadi meneo ya Amana, akaingia kwenye gari lake ambao alilipaki na kutokomea. Wala hakuhitaji kujua kama amekufa au la. Kwake kulenga shabaha ulikuwa ni mchezo mdogo sana.

Alianza kuwa mlenga shabaha akiwa na umri wa miaka minne tu, hivyo alikuwa na uhakika kuwa atampiga kichwani na hala hakuhitaji kupiga nyingine ya kuhakikisha kuwa amekufa.



# YJ awapa 'Kizaizai' Baba Levo, Billnas

STAA wa Bongo Fleva, Yakuti Joseph, maarufu kama YJ ametamba kutikisa chati za muziki na ngoma yake mpya 'Kizaizai' aliyowashirikisha Baba Levo na Billnas.

YJ ambaye amerejea nchini hivi karibuni akitokea Falme za Kiarabu na Malaysia, ameweka wazi kuwa video ya ngoma hiyo imefanyika Bongo na ughaibuni.

Akizungumza na BT jana, YJ amesema ndani ya Kizaizai Billnas na Baba Levo wameonyesha uwezo mkubwa na kuinogesha ngoma hiyo ambayo imetoka jana.

"Audio ameitengeneza Mr T Touch na video amefanya Hanscana hapa Bongo na nje ya nchi, kazi hii inaonyesha ukubwa wake. Video tayari imetoka na ipo kwenye chaneli yangu ya YouTube, hivyo naomba mashabiki waendelee kuiangalia" amesema YJ.

# Jelly Brown, Nestor watoa kitu 'Ndafa'

MSANII wa kizazi kipya mwenye makazi yake nchini Australia, Jelly Brown, amewaomba wapenzi wa muziki kupokea video ya wimbo wake mpya 'Ndafa' ambao umeanza kutikisa mitaani.

Akizungumza na BT, Jelly Brown amesema katika ngoma hiyo inayozungumzia malavidavi amemshirikisha mwanamuziki anayefanya vizuri kwa sasa, Nestor Again.

"Ndafa ni mwendelezo wa kazi zangu kubwa nilizotoa mwaka huu, naomba mashabiki waendelee kuniunga mkono ili nifike mbali zaidi, video tayari ipo kwenye chaneli yangu ya YouTube," amesema Jelly Brown.



HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FORSTER ATAJWA SPURS

GOLIKIPA wa England, Fraser Forster, 34, anaweza kuwa ameichezea Southampton mchezo wake wa mwisho huku mkataba wake ukimalizika mwishoni mwa msimu na akihusishwa na Tottenham. ***(Daily Echo)***

### CALVERT-LEWIN KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Everton na Timu ya Taifa ya England, Dominic Calvert-Lewin, 25, anatarajia kuondoka kwenye klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu huku Arsenal na Newcastle United zikionyesha nia ya kumtaka. ***(Football Insider)***

### GUNDOGAN ANUKIA MADRID

REAL Madrid wanaripotiwa kumtaka kiungo wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Ilkay Gundogan, 31. ***(Marca)***

### YAMBANA LINGARD

KLABU ya Newcastle United haitamsajili kiungo anayemaliza mkataba Manchester United, Jesse Lingard, vinginevyo kama atapunguza mshahara anaotaka wa pauni 150,000 kwa wiki. ***(ESPN)***

### UMTITI KUTUA ARSENAL

MLINZI wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Samuel Umtiti, 28, anaweza kutua Arsenal kwa mkopo. ***(Sport)***

### CHAMBAERLAIN HUYO SOKONI

LIVERPOOL inajiandaa kusikiliza ofa kwa ajili ya kiungo wake wa Timu ya Taifa ya England, Alex Oxlade-Chamberlain, 28, msimu huu. ***(ESPN)***

### POGBA KUTUA JUVE AU PSG

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba, 29, atajiunga na Paris St-Germain au Juventus mara atakapoondoka Manchester United bure msimu huu. ***(Eurosport)***

### BARCA KUMUUZA MINGUEZA

BARCELONA wanajiandaa kumuuza mlinzi wa kati wa kimataifa wa Hispania, Oscar Mingueza, 23, kipindi hiki cha majira ya joto, huku akitajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 4.2. ***(Sport)***

### JOHNSON KUTUA SPURS

TOTTENHAM Hotspur ni moja ya klabu zinazomtaka winga wa Nottingham Forest na Timu ya Taifa ya Wales, Brennan Johnson, 20. ***(Football. London)***

### WILLIAMS AWEKWA SOKONI

MANCHESTER United itasikiliza ofa kwa ajili ya beki wake wa kushoto, Brandon Williams, 21, msimu huu baada ya kuitumikia Norwich City kwa mkopo msimu huu. ***(Manchester Evening News)***

### GROSS, WELBECK MAMBO SAFI

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Pascal Gross, 30 na mshambuliaji wa England, Danny Welbeck mwenye miaka 31, wanakaribia kusaini mikataba mipya Brighton. ***(Argus)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RUDIGER AFUNGUKA SABABU KUONDOKA

Asema mazungumzo ya mkataba mpya yalianza kwa ugumu na kupelekea...

**LONDON,** England

ANTONIO Rudiger ameweka wazi sababu ya yeye kuondoka Chelsea mwishoni mwa msimu huu, akisema majadiliano ya mkataba wake yalianza kwa ugumu.

**Na sasa Rudiger atakuwa mchezaji halali wa Real Madrid kuanzia Juni Mosi, mwaka huu wakati sakata la kusaini mkataba mpya na Chelsea likitarajiwa kumalizika kwa kutofikia makubaliano wikendi hii.**

Kwa misimu miwili iliyopita, Rudiger amekuwa muhimili mkubwa katika kikosi cha Chelsea.

Uwezo wake wa kuiongoza safu ya ulinzi na timu kwa ujumla, ndani na nje ya uwanja, ni vitu vikubwa kwake.

Fununu za kuondoka kwake Stamford Bridge zilizua taharuki, kila mdau akitaka kujua ni kipi hasa kimepelekea sakata la mkataba mpya kutofikia makubaliano na sasa anaondoka akiwa mchezaji huru.

Akizungumza na BBC Sport, Rudiger ameweka wazi kilichotokea na kushindikana kusaini mkataba mpya.

"Kwa bahati mbaya, majadiliano ya mkataba wangu yalianza kuwa magumu. Biashara ni biashara lakini inapotokea hujasikia chochote kutoka kwenye uongozi wa klabu kuanzia Agosti hadi Januari, hali inabadilika.

"Baada ya ofa ya kwanza, kulikuwa na muda mrefu sana uliopita bila taarifa yeyote. Unajua, sisi sio roboti. Hauwezi kusubiri kwa miezi kadhaa bila kujua hatima yako ya mbele.

"Ni kweli, hakuna mtu alitarajia vikwazo vingetokea, lakini mwisho wa siku, klabu nyingine kubwa ziliyesha uhitaji na nilipaswa kufanya uamuzi. Nitaishia hapa kwa sababu ukiweka biashara pembeni, sina kitu chochote kibaya cha kusema kuhusu klabu hii."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 200,
MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
WOLVERHAMPTON
1 | 1.16
X | 6.71
2 | 13.82
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ALABA KUCHEZA FAINALI YA UEFA



**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amethibitisha, David Alaba atashiriki kwa "asilimia 100" kwenye mchezo wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Real Madrid itakapokutana na Liverpool wikendi ijayo.

Alaba amekuwa akiuguza jeraha la misuli ya paja alilolipata katika mchezo wa nusu fainali ya kwanza dhidi ya Manchester City mwezi uliopita na hakushiriki katika mchezo wa mwisho wa Madrid wa LaLiga msimu huu ilipokutana na Real Betis hapo juzi.


Los Blancos walitoka suluhu pale Santiago Bernabeu na Ancelotti alithibitisha baadaye kuwa beki huyo wa Austria atacheza dhidi ya Liverpool kwenye Uwanja wa Stade de France Jumamosi ijayo.

"Alaba atacheza fainali lakini haikuwa lazima kujitayarisha," alisema Ancelotti akiiambia Movistar+.

"Atacheza kwa asilimia 100 yuko fiti. Hajacheza tangu Aprili 26, ni kweli, lakini sio tu hali ya mwili inazingatiwa kwa mechi. Ustadi na uzoefu pia.

"Tunamhitaji zaidi kwenye fainali hii, hasa kutokana na uzoefu wake, hivyo naweza kuthibitisha kwa asilimia 100 atakuwepo."

Kocha huyo wa Italia anatarajia kuwa na Gareth Bale kwa mara nyingine kabla ya mkataba wake kumalizika mwishoni mwa msimu huu.



## Mbappe kuendelea na adhabu

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa PSG, Kylian Mbappe alipata adhabu kufungiwa mchezo mmoja wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Kwa mujibu wa sheria za Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA), inasema adhabu hiyo itachukuliwa kwenye ligi nyingine kama mchezaji huyo atahama msimu huu wa joto na atakosa mchezo mmoja.

Bado haijajulikana kama Mbappe atasalia Ufaransa na PSG au ataondoka kujiunga na Real Madrid.

Tetesi zinadai tayari amefikia makubaliano binafsi na mabingwa hao wa LaLiga na atatangazwa baada ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Katika dakika chache za mwisho za mechi ambayo mabingwa hao wa Ufaransa walishinda kwa ushindi mnono wa mabao 4-0, huku Mbappe akifunga bao, mshambuliaji huyo alipata kadi ya njano.

Adhabu hiyo ambayo imethibitishwa na Shirikisho la Soka la Ufaransa (FFF), itaanza kutekelezwa kuanzia wiki ijayo iwe atasalia au atahama.

,000,000



# KARIA AWATAKA MABINGWA SIMBA QUEENS WAJIPANGE

**Na Saada Akida**

RAIS wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia ameitaka klabu ya Simba kuhakikisha inasajili wachezaji wenye uwezo mkubwa na kukiimarisha zaidi kikosi cha Simba Queens kwa ajili ya kwenda kufanya vizuri katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yatakayofanyika baadaye mwaka huu.

**Mashindano hayo ya Ukanda wa CECAFA yatafanyika jijini Arusha, baada ya Tanzania kuthibitisha kuwa mwenyeji wa michuano hiyo huku Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan akitarajiwa kuwa mgeni rasmi siku ya fainali.**

Karia alisema hayo juzi baada ya kuikabidhi Simba Queens kombe la ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ambalo wamelichukua kwa mara ya tatu mfululizo.

Rais huyo alisema anataka kuona Simba Queens inafanya vyema kwenye michuano hiyo na kuleta heshima kwa Tanzania kubakisha kombe na zawadi.

Alisema Simba Queens wanatakiwa kuanza kujiandaa mapema na ligi hiyo kwa sababu msimu uliopita yalipofanyika jijini Nairobi, Kenya haikuwa na matokeo mazuri.

"Msimu uliopita hawakufanya vizuri na zawadi na ubingwa ukaenda Kenya, msimu huu Simba Queens wanatakiwa kufanya maandalizi mazuri na usajili kwa sababu Tanzania ni wenyeji wa michuano hiyo na tunataraja mama, Rais Samia ikimpendeza aka kuwa mgeni rasmi na kutoa zawadi kwa bingwa," alisema na alongeza;

"Kama Tanzania hatutaraji kuona zawadi hizo zikienda katika mataifa mengine, Simba Queens wanatakiwa kujipanga vizuri kuhakikisha zawadi hizo zinabaki nyumbani na isije kutoka kwenda ugenini," alisema Karia.



Wachezaji wa Simba Queens, wakiwa na kombe lao walilokabidhiwa baada ya kuibuka mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu wa 2021/2022 uliomalizika juzi. Katika mechi ya funga dimba mabingwa hao mara tatu mfululizo waliifunga Baobab Queens mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzales alisema tayari wamepokea ripoti kutoka benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Sebastian Nkoma na wanatarajia kuanza usajili mapema mwezi ujao.

Barbara alisema wamejipanga kusajili nyota wapya ambao watakiimarisha kikosi chao kwa ajili ya kulibakisha nchini taji la Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake.

"Baada ya kukamilisha usajili, ambao majina ya baadhi ya nyota tunaowahitaji tumeshayapata, kikosi kitaelekea Arusha kuweka kambi ya kujiandaa na michuano hiyo inayotarajia kutimua vumbi ifikapo Agosti, mwaka huu," alisema Barbara.

Aliongeza hawataki kurudia makosa waliyofanya msimu uliopita na anaamini hawatawaangusha Watanzania katika michuano ya mwaka huu.



# *Coastal Union yamhofia Sopu*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union imesema haina uhakika kama mchezaji wake, Abdul Suleiman 'Sopu' atabakia katika kikosi hicho kwa ajili ya msimu ujao kutokana na kuonyesha kiwango kikubwa msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaoelekea ukingoni.

Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda (pichani), alisema mara baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji kumalizika na wao kupata ushindi wa mabao 2-1, hana imani kama watafanikiwa kumbakisha nyota huyo.

Mgunda alisema Sopu ambaye alifunga mabao yote mawili ya timu yao, amekuwa na kiwango kikubwa katika msimu huu, hivyo anaweza 'kubebwa' na klabu kubwa.

"Sopu ana kiwango kikubwa, ni mchezaji mzuri na amekuwa na mwendelezo mzuri pia, niseme tu kubaki au kutobaki Coastal kunategemea na wenye visu vikali, siku zote mwenye kisu kikali ndiye anayekula nyama. Sisi inawezekana tukawa tunataka abaki, lakini mwenye kisu kikali anakuja, anataka kumchukua, huwezi kumzuia, na hawa vijana hii ndiyo kazi yao na maisha yao," alisema Mgunda.

Kabla kujiunga na Coastal Union, mchezaji huyo alikuwa akiichezea Ndanda kwa mkopo akitokea kwenye kikosi cha pili cha Simba.


JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/05/22 | 18:00 | Crystal Palace vs Manchester Utd | 2.89 | 3.32 | 2.31 |
| 02. 22/05/22 | 18:00 | Brentford vs Leeds | 2.28 | 3.42 | 2.87 |
| 03. 22/05/22 | 18:00 | Burnley vs Newcastle | 2.34 | 3.22 | 2.92 |
| 04. 22/05/22 | 18:00 | Brighton vs West Ham | 2.45 | 3.30 | 2.71 |
| 05. 22/05/22 | 18:00 | Brondby vs Silkeborg | 2.48 | 3.59 | 2.54 |
| 06. 22/05/22 | 18:30 | Kalmar vs Djurgardens IF | 2.77 | 2.97 | 2.48 |
| 07. 22/05/22 | 18:30 | Elche vs Getafe | 3.05 | 2.95 | 2.49 |
| 08. 22/05/22 | 19:00 | Stromsgodset vs Valerenga | 2.64 | 3.29 | 2.54 |
| 09. 22/05/22 | 19:00 | Jerv vs Odd Ballklubb | 2.90 | 3.25 | 2.37 |
| 10. 22/05/22 | 21:00 | Ham-Kam vs Rosenborg | 2.53 | 3.27 | 2.68 |
| 11. 22/05/22 | 23:00 | Real Sociedad vs Atletico Madrid | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 12. 22/05/22 | 23:00 | Barcelona vs Villarreal | 2.47 | 3.60 | 2.58 |
| 13. 22/05/22 | 23:00 | Sevilla FC vs Athletic Bilbao | 2.35 | 3.35 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 22/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 5557 | Spezia vs Napoli | 5.35 | 4.36 | 1.51 |
| 14:00 | 2780 | Landskrona Bois vs IK Brage | 3.03 | 3.48 | 2.26 |
| 14:00 | 4162 | Dalkurd FF vs Vasteras SK | 2.77 | 3.53 | 2.40 |
| 16:00 | 1274 | Trelleborgs FF vs Osters IF | 2.45 | 3.17 | 2.97 |
| 16:00 | 2962 | Elfsborg vs IFK Goteborg | 1.50 | 3.98 | 5.44 |
| 16:00 | 3155 | Basaksehir vs Trabzonspor | 1.83 | 3.59 | 3.99 |
| 16:00 | 3161 | Lahti vs AC Oulu | 2.00 | 3.31 | 3.35 |
| 16:00 | 4371 | Varbergs Bois vs Degerfors | 1.88 | 3.41 | 3.65 |
| 16:00 | 5333 | Hammarby vs Norrkoping | 1.77 | 3.60 | 3.89 |
| 16:00 | 5520 | Fatih Karagumruk vs Alanyaspor | 3.03 | 3.57 | 2.15 |
| 17:00 | 5981 | Ismaily SC vs National Bank | 2.44 | 2.84 | 3.19 |
| 18:00 | 2398 | Liverpool vs Wolverhampton | 1.16 | 6.71 | 13.82 |
| 18:00 | 2963 | Brighton vs West Ham | 2.47 | 3.32 | 2.67 |
| 18:00 | 3235 | Burnley vs Newcastle | 2.32 | 3.26 | 2.92 |
| 18:00 | 3692 | Brondby vs Silkeborg | 2.31 | 3.63 | 2.73 |
| 18:00 | 4099 | Copenhagen vs Aalborg | 1.48 | 4.38 | 5.78 |
| 18:00 | 4832 | Chelsea vs Watford | 1.15 | 6.95 | 14.88 |
| 18:00 | 5040 | Manchester City vs Aston Villa | 1.19 | 6.25 | 13.02 |
| 18:00 | 5085 | Arsenal vs Everton | 1.57 | 4.05 | 5.08 |
| 18:00 | 5169 | Leicester vs Southampton | 1.88 | 3.77 | 3.52 |
| 18:00 | 5616 | Midtjylland vs Randers | 1.64 | 4.17 | 4.46 |
| 18:00 | 5628 | Brentford vs Leeds | 2.28 | 3.47 | 2.83 |
| 18:00 | 5719 | Crystal Palace vs Manchester Utd | 2.89 | 3.33 | 2.31 |
| 18:00 | 5869 | Norwich City vs Tottenham | 10.87 | 6.32 | 1.21 |
| 18:15 | 5446 | Bromley vs Wrexham | 4.85 | 3.78 | 1.59 |
| 18:30 | 1799 | HJK Helsinki vs Haka | 1.44 | 3.99 | 6.43 |
| 18:30 | 2348 | Malmo vs BK Hacken | 1.87 | 3.41 | 3.66 |
| 18:30 | 3768 | Kalmar vs Djurgardens IF | 3.17 | 2.97 | 2.23 |
| 18:30 | 4385 | Elche vs Getafe | 3.06 | 2.91 | 2.50 |
| 19:00 | 1022 | Sarpsborg vs Aalesunds | 1.74 | 3.74 | 4.28 |
| 19:00 | 1818 | Inter vs Sampdoria | 1.11 | 8.33 | 16.85 |
| 19:00 | 2901 | Tromso vs Viking | 2.98 | 3.33 | 2.28 |
| 19:00 | 3079 | Stromsgodset vs Valerenga | 2.49 | 3.30 | 2.70 |
| 19:00 | 3448 | Jerv vs Odd Ballklubb | 2.77 | 3.27 | 2.45 |
| 19:00 | 3572 | Adana Demirspor vs Goeztepe | 1.40 | 5.00 | 6.20 |
| 19:00 | 3707 | Sassuolo vs AC Milan | 5.75 | 4.76 | 1.44 |
| 19:00 | 4053 | Pafos FC vs Apoel Nicosia | 6.80 | 4.20 | 1.46 |
| 19:00 | 5050 | Haugesund vs Bodo Glimt | 3.82 | 3.53 | 1.89 |
| 19:15 | 4510 | Porto vs Tondela | 1.17 | 6.24 | 11.70 |
| 19:30 | 5782 | Brugge vs Anderlecht | 2.05 | 3.68 | 3.18 |
| 21:00 | 2134 | Granada vs Espanyol | 1.44 | 4.51 | 6.42 |
| 21:00 | 4891 | Osasuna vs Mallorca | 3.35 | 3.30 | 2.14 |
| 21:00 | 5742 | Alaves vs Cadiz CF | 4.09 | 3.59 | 1.83 |
| 22:00 | 1249 | Salernitana vs Udinese | 1.68 | 3.92 | 4.37 |
| 22:00 | 1801 | El Ittihad Alexandria vs Pyramids | 4.57 | 3.33 | 1.80 |
| 22:00 | 2300 | Venezia vs Cagliari | 4.55 | 3.86 | 1.66 |
| 23:00 | 1777 | Barcelona vs Villarreal | 2.04 | 3.82 | 3.14 |
| 23:00 | 2136 | Montreal Impact vs Real Salt Lake | 1.80 | 3.58 | 4.43 |
| 23:00 | 2935 | Sevilla FC vs Athletic Bilbao | 2.45 | 3.20 | 2.85 |
| 23:00 | 3442 | Real Sociedad vs Atletico Madrid | 2.64 | 3.19 | 2.64 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Mei 22, 2022

Nipashe




Rudiger afunguka sababu kuondoka UKURASA 21



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa (watatu kulia), akimkabidhi Miss Tanzania 2022, Halima Kopwe hundi ya mfano ya Sh. milioni 10 baada ya kutangazwa mshindi katika shindano hilo lililofanyika usiku wa kuamkia jana kwenye Ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA, GEITA GOLD MECHI YA HESHIMA

**Na Adam Fungamwanngo**

## ●●● Pablo aahidi furaha akirejea CCM Kirumba kwa mara ya...

MABINGWA watetezi, Simba wanatarajia kukutana na wenyeji Geita Gold FC kutoka mkoani Geita katika mechi ya kusaka heshima ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

**Simba ambayo kwa sasa ni kama mtu anayepigania roho yake, itahitaji kupata ushindi ili kujiimarisha katika nafasi ya pili lakini ikiiombea Yanga kupata matokeo mabaya kwenye michezo yake iliyosalia na kuuhifadhi ubingwa wake.**

Kimahesabu inawezekana, lakini kiuhalisia, hata Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco na Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally kwa nyakati tofauti wameonekana kukata tamaa ya kutetea ubingwa wa ligi hiyo wakisema ni jambo ambalo si rahisi sana.

Hata kama haiwazii ubingwa, lakini Simba itakuwa ina kazi moja ya kusaka ushindi ili kuwafurahisha mashabiki wake wa mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa kumaliza msimu huu kwa heshima.

Pablo alisema amefurahi kurejea tena Mwanza kwani mechi yake ya kwanza baada ya kutua Tanzania na kuanza kibarua cha kuifundisha Simba ilikuwa kwenye uwanja huo ambapo walikutana na Ruvu Shooting, akipata ushindi wa mabao 4-1.

"Nafurahi nimerudi Mwanza, mechi yangu ya kwanza nchini Tanzania ilikuwa hapa Mwanza na tulicheza vizuri. Nimeiona Geita Gold ikicheza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ni timu nzuri na nilisema siku chache nyuma kuwa ndiyo ilistahili kucheza nasi nusu fainali ya Kombe la FA, najua uwanja hauko vizuri na ndiyo tunacheza hata kwenye mechi ya nusu fainali dhidi ya Yanga, lakini tumejiandaa kupambana katika mechi hii," alisema Pablo.

Kocha Msaidizi wa Geita Gold, Mathias Wandiba amesema watashuka uwanjani kucheza na Simba iliyo na wachezaji bora, lakini na wao wana wachezaji imara.

"Timu bora ni lazima uifunge timu bora, tunataka tupate ushindi ili tutimize malengo tuliojiwekea. Naamini tunakutana na Simba iliyo na wachezaji bora, lakini tunakwenda na sisi tuna wachezaji imara, vijana na wazoefu, tumewaandaa ndani ya uwanja kiufundi na kisaikolojia pia, naamini tutakwenda kufanya vizuri na kubakisha pointi tatu kwenye uwanja wetu wa nyumbani," alisema kocha huyo.

Nahodha Msaidizi wa Geita Gold, Maka Edward amesema walimu wameshatimiza majukumu yao na sasa kazi kubwa imebaki kwa wao wachezaji kutekeleza mafunzo waliyopewa kwa vitendo.

"Kabla hata walimu hawajasema, kila mchezaji anajua anakwenda kucheza mechi ya aina gani dhidi ya Simba, morali iko juu na kila mchezaji ana ari ya kupambana. Kila mchezaji anajua kucheza vizuri mechi hizi, basi kuna uwezekano wa kusongea mbele, kuna uteuzi kwenye timu ya taifa, na pia kwenda kwenye klabu nyingine kubwa zaidi," alisema nahodha huyo.

Kikosi cha Simba kiliwasili Mwanza tangu juzi tayari kwa mchezo huo wa raundi ya 23.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba yenye pointi 50 ipo kwenye nafasi ya pili ambayo imekuwa ni kama ya kudumu wakati Geita Gold yenyewe iko katika nafasi ya nne baada ya kujikusanyia pointi 34.

Ligi hiyo inayotoa wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa itaendelea tena kesho kwa Dodoma Jiji kuwakaribisha Namungo kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma wakati Yanga itawafuata Biashara United kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.

# Yanga kazi bado haijakwisha Bara

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

BAADA ya timu yake kupata ushindi mnono wa mabao 4-0, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, amesema hafikirii lini watatangazwa mabingwa zaidi ya kuendelea kuwapa wachezaji wake mazoezi mengi yenye mbinu mpya na kupunguza makosa kwa ajili ya kuongeza ubora wa nyota wake.

Nabi aliliambia gazeti hili anahitaji kuona timu yake inavuna pointi tatu muhimu kutoka katika kila mechi zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo alisema anataka kuona nyota wake wanakuwa makini na mafunzo anayowapa katika mazoezi na kuhakikisha hawafanyi makosa na kila timu wanayokutaka nayo wanaipa heshima bila kujali nafasi waliyopo kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Mara nyingi mazoezi ya mbinu ambayo tunafanya yanalingana na wapinzani tunaoenda kukutana nao, bahati nzuri timu tano tulizobaki kucheza nazo, kwenye mzunguko wa kwanza nyingi tulipata matokeo mazuri dhidi yao na tunawafahamu," alisema na aliongeza;

"Hatutakiwi kuridhika haraka ukizingatia wapinzani wetu watakuja kivingine kama ilivyokuwa katika mchezo wa leo (juzi), dhidi ya Mbeya Kwanza, walianza vizuri lakini walifanya makosa na kufanikiwa kupata bao la kwanza dakika 37 na kufungua njia zao na kupata magoli mengine," alisema Nabi.

Alisema hakuna mechi ambayo ni rahisi, jambo ambalo amekuwa akiwasisitizia wachezaji wake kuongeza umakini ili mbinu anazotoa mazoezi ziweze kufanya kazi ya kuvuna pointi tatu iliyokusudiwa.

"Ushindi wa mchezo huu utanisaidia kuwapa nafasi ya wachezaji wangu waliocheza muda mrefu kupumzika ili kujiandaa na mchezo wa nusu fainali, kuhusu Salum Abubakar hakucheza kwa kiwango kikubwa kwa sababu mechi yetu dhidi ya Dodoma Jiji FC alitumia nguvu kubwa," alisema Nabi.

Naye Kocha Msaidizi wa Mbeya Kwanza, Shija Renatus, alisema mambo matatu yaliyosababisha kupoteza mechi hiyo dhidi ya Yanga ni uchovu wa safari waliokuwa nao wachezaji wake lakini pia kurudishwa nyuma siku moja kwa mchezo huo ambao awali ulitakiwa kuchezwa jana.

Shija alisema pia tofauti ya ubora wa kikosi chao na Yanga ambao wako katika mbio za ubingwa kwa kucheza kwa mfumo mwingine wasioufahamu kuliwapoteza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >